

NENDENI, MKAWAAMBIE

WANAFUNZI WANGU



Ni majaliwa, kwa kweli, kuja kwenye nyumba ya Mungu mapema asubuhi hii, na kumwabudu Bwana wetu, Kristo wetu aliyefufuka. Loo, ilikuwa... Ndio kwanza niingie, muda mfupi uliopita. Tulikuwa na mkutano wa ajabu sana wa kimishenari jana usiku, mkutano mkubwa, uliohubiriwa moja kwa moja mpaka karibu usiku wa manane. Na tumeamka asubuhi ya leo kumwabudu Bwana wetu Yesu Kristo. Ni ajabu jinsi gani kukusanyika pamoja, kukutana!

² Kama vile Ndugu Thom alivyokuwa akisema tu, leo ilikuwa ndiyo siku ambayo Yeye alithibitisha kile alichokuwa. Mtu yeyote angeweza kufa, lakini ilimchukua Mungu kufufuka tena. Maishani Mwake, Yeye alionekana kama Mungu, alihubiri kama Mungu, aliponya kama Mungu, alitenda kama Mungu. Alikuwa ni Mungu. Naye akathibitisha kwenye asubuhi ya Pasaka ya kwamba alikuwa Mungu. Alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Yeye hakuwa nabii, hata hivyo alikuwa Nabii. Alikuwa mtu mwema, lakini hata hivyo alikuwa zaidi ya mtu mwema. Alikuwa Mungu. Na kwa hiyo hii ndiyo siku, katika ukumbusho wa kufufuka Kwake, ambayo alilithibitisha.

³ Inatupasa kufanya ziara asubuhi ya leo, na tushuke kufuata Mto Ganges, mngekutana na akina mama huko wakiwatoa watoto wao kafara kwa ngwana, mamba, wanawazamisha. Ati unanena juu ya uaminifu? Wanawachukua watoto wao wanene na kuwavurumisha huko nje mamba wapate kuwaponda-ponda. Huo ni uaminifu mkubwa.

⁴ Kama tungeshuka kupitia India, leo, mngekuta, kandokando ya barabara, watu wengi labda wamejilaza kwenye misumari, wakitembea kwenye moto, na kujitesa kwa namna fulani. Baadhi yao, bila shaka, wanafanya ucheshi tu, kwa sababu ni kwa ajili ya watalii. Lakini huko nyuma barani kuna mtu halisi ambaye amelala huko nyuma, akijitesa, akifikiri kwamba anaweza kupata raha na amani, omba—akimwomba Muhammed.

⁵ Tamasha ya kusikitisha, hivi majuzi, alipokuwa akipanda Golgotha, kuingia mji wa... nje ya mji wa Yerusalemu, hasa. Kulikuwako pale pale mahali pa kusulubishwa, kwenye makaburi ya Kiislamu, alilala mwanamke chini ya lundo dogo la magugu aliyokuwa ametandaza pale, akiwa na kipande kikuukuu cha mkate mweusi. Alikuwa amelala pale kwa siku kadhaa, akiililia nafsi ya mpendwa wake aliyekuwa

amemwacha; moja kwa moja mahali uliposimama msalaba. Na, kwa hiyo, kuona ulimwengu katika hali yake ya kikafiri!

⁶ Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Gadus, si muda mrefu uliopita, alikuwa amerudi kutoka China hivi punde. Alisema, “Ndugu Branham, lilikuwa jambo la kusikitisha kuona, kule Uchina.” Kasema, “Baadhi yao labda wameinua mikono yao juu kadiri ya muda wa miaka minne, mfululizo, mpaka kucha zao za vidole zikaota kupitia mikononi mwao, zikatokeza upande wa nyuma. Akisema, ‘Kamwe sitauondoa mkono wangu mpaka utakaponipa amani nafsi mwangu, Budha mkuu.’”

⁷ Na—na halafu wengi wa watoto wadogo, wakiwa wachanga, wanaivunja miguu yao kwenye tao, namna *hii*; na kuvaa kiatu cha namba mbili au tatu tu, maisha yao yote; miguu mifupi sana, kwa sababu wanamtolea sadaka mungu fulani wa kikafiri.

⁸ Nimeyatembelea makaburi ya karibu waanzilishi wote wa dini; Muhammed, na pia kwe—kwenye kaburi la Budha, na Confucius, na wengi wa wanafalsafa.

⁹ Lakini, leo, zaidi ya yote, sisi Wakristo tunaweza kutupa vichwa vyetu nyuma na kuimba, “Yu hai, Yu hai, Kristo Yesu yu hai leo. Huenda ukaniuliza jinsi ninavyojua Yu hai; anaishi moyoni mwangu.” Nasi tuna kaburi tupu leo hii.

¹⁰ Yapata miaka miwili iliyopita nilikuwa nikienda kwenye kaburi, mapema sana asubuhi moja, kuweka ua kwenye kaburi la mama wa mvulana wangu mdogo, ambaye ametuacha, na dada yake mdogo ambaye amewekwa juu ya mkono wake, hapa nje kwenye Makaburi ya Walnut Ridge. Basi alipokuwa akipita, huko jamaa mdogo aliguna, mara mbili au tatu, huku akilia, akileta chungu kidogo cha maua. Tukapiga magoti pale, tukavua kofia zetu; na kuyaweka juu ya hilo kaburi, kando ya kaburi. Nami nikainua mkono wangu, na kumkumbatia.

¹¹ Nikasema, “Billy, yule pale mama yako na dada yako mdogo. Mwili wao umelazwa hapa chini. Nafsi zao, katika Uwepo wa Mungu. Lakini ng’ambo ya bahari, kule, kuna kaburi tupu leo, ambalo ni kumbukumbu kwa Wakristo wote. Yeye yu hai.” Yu hai. Huo ndio msingi asili wa—wa imani yetu ya Kikristo, kwamba Yesu Kristo yu hai leo.

¹² Sasa, kama ilivyoandikwa kwenye gazeti...Sasa, kwa kawaida, kwenye ibada yetu ya mapambazuko ya Pasaka, kwa kawaida huwa na wi—wimbo mmoja au mbili, na kuweka muda mwingi zaidi hapa Maskanini... Ikitokea kuna wageni pamoja nasi, vema, wakati wetu mwingi sana hapa upo kwenye Neno. Sisi ni watu hodari kuliadini Neno la Mungu. Na kimsingi, nafikiri, hiyo ndiyo njia na hapo ndipo mahali palipo sahihi. Na leo hii nina ma—mambo fulani muhimu sana ninayotaka kuzungumzia, ya ufufuo, mambo fulani ya kimsingi. Nami ninataka kuandika mambo fulani chini, mimi mwenyewe, ninapoendelea.

¹³ Kwanza, hebu tufungue hapa katika Maandiko, katika Mathayo mlango wa 24, ama mlango wa 22, hasa, na kuanzia kwenye kifungu cha 41. Ninataka kusoma fungu la Maandiko, kisha niuendee ufufuo. Kiini changu cha ibada asubuhi ya leo, kiko hapa. “Wakati Mafarisayo walipokuwa wamekusanyika pamoja...” Samahani. Ni—nilifungua mahali pabaya, katika kusoma kwangu kwa hili fungu. Ilikuwa—ilikuwa ni Mathayo m—mlango wa 23, ninaamini... Hebu kidogo. Kunradhi, kwamba, niliingia nimechelewa jana usiku wala sikuweza kuliandaa somo langu sawasawa, asubuhi ya leo, mahali pa kupata somo langu la Maandiko. Loo, naam.

*...nendeni mkawaambie mwanafunzi wangu
kwamba nitakutana nao huko Galilaya,...*

¹⁴ Vema, bwana. Sasa, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu alitoa agizo hapa kwa maskini wanawake hawa, baada ya kufufuka Kwake, kwamba Yeye alikuwa... kile alichopaswa kufanya. Alitakiwa kuwaambia kwamba atakutana nao huko Galilaya, ambako aliwaahidi kwamba—kwamba ange—angewatokea, na kwamba angekuwa pamoja nao daima.

¹⁵ Sasa katika mlango wa 28 wa Mathayo, hasa, na kuanzia kifungu cha 7, tunasoma.

*Nanyi nendeni upesi mkawaambie wanafunzi
wake kwamba amefufuka katika wafu; na,
tazama, anawatangulia kwenda Galilaya; ndiko
mtakakomwona: haya, nimekwisha waambia.*

¹⁶ Ulikuwa ni ujumbe wa Malaika kwa wanawake, kwa Mariamu na...wale Mariamu wawili. Ilikuwa kwenye... asubuhi ya kwanza ya Pasaka; habari tukufu ilikuwa imetangazwa.

¹⁷ Alipoishi hapa duniani, Yeye alitembea kama Mwanadamu, alionekana kama Mwanadamu. Alikuwa na utu Wa—Wake wote wa nje kama Mwanadamu; hata hivyo, kwa ndani, Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Alikuwa ni Imanueli. Leo hii ni kumbukumbu la tukio kubwa sana lililopata kutokea katika ulimwengu mzima. Hapakuwahi kuwa na mtu, nje ya Mtu huyu, Kristo Yesu, aliyesema, “Ninao uwezo wa kuuweka chini uhai Wangu, na nina uwezo wa kuutwaa tena.”

¹⁸ Confucius, naam, na Muhammed, na Budha, wengi wa hao wengine, walikuwa wanafalsafa mashuhuri; lakini, walipokufa, hilo lilitosha. Walikwisha milele. Waliwazika, na hilo...hilo lililimalizia.

¹⁹ Lakini Mtu huyu alikuwa na uwezo wa kuuweka chini uhai Wake na kuuinua tena. Mtu pekee ambaye angeweza kuifanya hivyo; Mtu pekee aliyekuwa nao, aliyepata kuthibitisha ya kwamba angeweza kufanya hivyo.

20 Na, sasa, na imekuwa ndiyo hofu ya mwanadamu, kote katika nyakati, ilikuwa ni mauti. Kila mtu aliyekuja ulimwenguni sikuzote aliogopa mauti. Wakuu. . . Tumekuwa na kina Napoleon, tumekuwa na kina Hitler, na kila kitu; lakini inapofika saa ya kufa, kila mmoja wao anasinyaa. Nimewasikia watu wakinena na kujivunia mambo makubwa ya kukufuru; lakini, inapofikia mauti, wao, kila mmoja, anasinyaa.

21 Kama vile Bob Ingersoll, yule kafiri mashuhuri sana, alipotoa saa yake na kuwaonyesha jamaa zake, na kusema, “Kama kuna Mungu, nitakufa katika dakika moja, kutoka kwenye pigo la saa hii.” Kisha, baada ya hiyo dakika kupita, hakufa kamwe. Akafanya “ha-ha” kubwa mno, na neno, na kusema, “Mnaona, hakuna kitu kama Mungu.” Lakini wakati. . .

22 Bila shaka, hiyo ilikuwa tu kuyatimiza Maandiko. Maandiko yalisema ya kwamba, kwamba, “Wenye kudhihaki watakuja katika siku za mwisho,” nasi tunao.

23 Kwa hiyo akasema, “Sasa, mnaona, hakuna kitu kama Mungu.” Lakini katika chumba cha hospitalini alipokuwa mahututi, ambamo wengi walikuwa wamekusanyika kuona kitakachotukia, alilia kwa sauti, “Ee Mungu, uirehemu nafsi yangu!”

24 Baba yangu alikuwa rafiki msiri sana wa. . . au, si rafiki msiri, hasa, wa kafiri mashuhuri. Naye akasema, “Hakuna kitu kama Mungu.” Alilaani mawazo yenyewe ya Mungu. Mkewe angefunganisha mkokoteni na kwenda kanisani, naye angetoka aende kulima mahindi yake Jumapili, na kila kitu, ili tu kuonyesha kwamba hapakuwapo na kitu kama Mungu.

25 Siku moja, alikuwa ndio kwanza ametoka tu kuanika ngano yake, na kuiweka yote matita; radi ikaipiga, ikaiteketeza yote. Alitoka huko nje na kuinua mkono wake na kuyalaani mawazo yenyewe ya Mungu. Basi, alipofanya hivyo, basi radi ikapiga banda lake ambamo alikuwa na farasi wazuri wa mbio, na kuwaua, kila mmoja.

26 Halafu majuma machache baada ya hapo, akalazwa chini akiugua homa ya matumbo, ndipo akafa, huku baba yangu akisaidia kumshikilia kitandani. Naye akapiga mayowe na kulia, pepo, huku amefungwa minyororo, walikuwa wakija kumchukua, na kadhalika. Basi alipokaribia kuondoka, aliikusanya familia yake pamoja, watoto wake wadogo. Akasema, “Msithubutu kupitia njia ambayo baba yenu amepitia. Pitieni njia mama yenu anayopitia, kwa kuwa hiyo ndiyo njia pekee ya Uzima.”

27 Nina kitabu nyumbani, nacho kinatoa ushuhuda wa watu wengi mashuhuri, kama vile mkuu. . . mmoja wa malkia wakuu wa—wa Uingereza, na baadhi ya watu wengine. Walipokuwa wakiingia mautini, walipiga mayowe na kulia.

28 Malkia Elizabeth, wa Uingereza, alisema, “Laiti ningekuwa tu na . . . Ningeutoa ufalme wangu kama ningalikuwa na dakika tano za kuishi, ili nipate kutubu, na kuufanya moyo wangu kuwa sawa na Mungu.”

29 Mtu mwingine mashuhuri alisema, “Ninaingia gizani. Sijui niendako. Ningeweza. . .”

30 Ndipo kafiri mwingine mashuhuri akanena, akasema, “Inaonekana kuna kuta mbili, nami nikapiga makelele, na,” kasema, “ni kurudishwa tu mwangwi ukuta kwa ukuta.” Huo tu ndio alioweza kusikia. Alikuwa ameahirisha siku ya wokovu hata ikawa imechelewa kupita kiasi.

31 Kisha ninawawazia watu wakuu, mashuhuri, ambao walikufa, wakimwamini Bwana wetu Yesu Kristo na kufufuka Kwake. Nawazia, hapa, juu ya—ya D. L. Moody, wakati wa kifo chake, wengi wamesema. “Mbona, ati haya ni mauti?” Akasema, “Hii ndiyo siku yangu ya kupandishwa cheo.” Nami nikawazia, wakati—wakati John Wesley, wakati alipokuwa akifa. Wakati Abraham Lincoln alipopigwa risasi na alikuwa akitokwa na damu hata kufa, akiwa amelala ma—mahali fulani.

32 Nilipita karibu na jumba la makumbusho, na huku Illinois hapa, siku moja. Nikamwona mzee mweusi mwenye mzingo mdogo wa nywele nyeupe kukizunguka kichwa chake, akitembea huku na huku, akiangalia. Baada ya muda kidogo akasimama, na machozi yakatiririka mashavuni mwake. Akarudi nyuma na kuanza kukariri maombi. Nikamwangalia kwa dakika chache. Nilikuwa nikitembea, pia, kwa hivyo nikamwendea na kusema, “Mjomba, kuna nini? Naona unaomba.”

Akasema, “Angalia, iliyowekwa pale.”

33 Vema, nikaangalia iliyowekwa pale, na kitu pekee nilichoweza kuona kilikuwa ni nguo. Naye akasema . . . Nikasema, “Kitu pekee ninachokiona ni nguo.”

34 “Lakini,” kasema, “angalia, bwana.” Akasema, “Chini ya koti langu kuna kovu la mshipi wa utumwa.” Akasema, “Na hiyo ni damu ya Abraham Lincoln.” Akasema, “Iligharimu damu ya Abraham Lincoln kuutoa mshipi huo wa utumwa kwangu.”

35 Nikawazia, “Kama ingemsisimua mtu mweusi, kwa sababu ya hiyo damu ya Abraham Lincoln, kwa sababu ilitoa mshipi wa utumwa kwake; Damu ya Yesu Kristo inapaswa kumaanisha nini kwa mwaminio, tunapotazama kule nyuma Kalvari na kuona pale ya kwamba aliutoa mkanda wa utumwa wa dhambi kutoka miyoni mwetu, na kutuweka huru,” ambao tumekuwa tukiuzungumzia, siku chache zilizopita usiku. Ni tofauti jinsi gani!

36 Abraham Lincoln, alipokuwa akifa, alikuwa ameufikia mwisho wake. Na wakati yeye . . . lakini alipopigwa risasi pale, katika kanisa hili kuu, naye alikuwa yuafa kitandani

mwake, alisema, “Ugeuzeni uso wangu kuelekea machweo ya jua.” Jua lilikuwa likitua jioni. Lincoln alikuwa akipumua, nayo damu ikibubujikia mapafuni mwake. Daima alikuwa amemtumainia Mungu. Akasema, “Ishikilieni mikono yangu juu.” Naye akauinua mkono wake. Akasema, “Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe,” wakati akiinamisha kichwa na kukata roho.

³⁷ Paul Rader, rafiki yangu msiri, aliyelandika wimbo wangu rasmi, *Amini Tu*; alipokuwa akifa kule, alikuwa ndio kwanza aegemeze bega lake, kichwa juu ya bega la meneja wangu, Bw. Baxter. Alikuwa mtu hodari sana ambaye alikuwa amesafiri baharini na nchi za ng'ambo, na kila kitu, naye alikuwa amechangamana huko nje, na kuchangamana na baadhi ya watu wa kimsingi, nao ujumbe wake ukamtia wasiwasi hata kufa. Ndipo alipokuwa akifa, alikuwa amelala chumbani, mahututi, alikuwa akihangaika sana.

³⁸ Basi huu hapa ushindi wa kweli wa mtu. Sikuzote alikuwa mcheshi mashuhuri, Paul alikuwa mcheshi mashuhuri, kama wengi wenu mlivyomjua. Walikuwa na kundi la waimbaji wanne kutoka kwenye maskini Chuo cha Biblia cha Moody kule chini. Nao walikuwa wameshusha mapazia kabisa, madirishani, alipokuwa akiondoka. Akainuka, akatazama. Akatikisa kichwa chake, akasema, “Kwani ni nani anayekufa, mimi au ninyi?” Kasema, “Fungueni mapazia hayo, na mkaniimbie nyimbo nzuri changamfu za Injili, za ufufuo.”

³⁹ Ndipo walipoanza kuimba namna hiyo, yeye alisema, “Yuko wapi ndugu yangu, Luke?”

⁴⁰ Wakamleta ndugu yake. Luke aliambatana naye kama vile mvulana wangu anavyoandamana nami, na kadhalika. Luke alikuwa katika chumba kingine, akilia. Luke akaingia; mtu mkubwa sana mwenye mabega mapana, pengine mnamfahamu. Yeye na Ma Sunday, na hao wote, walikuwepo.

⁴¹ Alipogeuka, alimshika Luke mkono, akasema, “Luke, tumetoka mbali pamoja. Lakini, liwazie, katika dakika tano kutoka sasa, nitakuwa nimesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake.”

Maisha ya watu mashuhuri yote
yanatukumbusha

Tunaweza kufanya maisha yetu adhimu,
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu;

Kumbukumbu, ambazo labda mtu mwingine,
Akisafiri juu ya bahari adhimu ya maisha,
Ambapo ndugu mpweke aliyeharibikiwa na
meli,
Akiona, atajipa moyo tena.

⁴² Ninawazia juu ya *Zaburi ya Maisha*, yule bingwa mtunga mashairi wa Kiingereza, Longfellow, alipoiandika. Nilisimama kando ya kaburi lake, hapa miezi michache iliyopita. Nikawazia juu ya ushairi wake mkuu na yale aliyokabidhi ulimwengu, nami... Hiyo *Zaburi Ya Maisha* ilikuwa ni mojawapo ya yale ninayoyapenda sana. Sikuzote mauti yalikuwa ni hofu. Mwanadamu aliyaogopa, kote kote tangu mwanzo. Huko nyuma kabisa, kutoka katika bustani ya Edeni, mwanadamu aliogopa mauti.

⁴³ Ninawazia juu ya yule nabii mkuu, Ayubu, alipoketi pale wakati huo naye alijua anaondoka. Alinena juu ya yale mahubiri makuu pale, ambayo tunapata kutoka Ayubu 14. Jinsi alivyoyatazama maua; jinsi yalivyokufa na kufufuka tena. Jinsi alivyoangalia miti; ikivuma, inabomoa, upepo huipasua. “Katika mauti, hata hivyo inaishi tena,” akasema. “Kupitia matone machache ya—ya maji, naam,” anasema, “inaishi.” Tunawaangalia wanyama we—we—wetu, na kadhalika, wanavyoishi na kufa. Kila kitu kinachoweza kusonga, kinapokufa, hakiishi tena.

⁴⁴ Kwa hiyo Ayubu alishangaa ilikuwaje Mungu angeweza kuchukua ua na kulifanya hai tena, na hata hivyo yeye asingeweza kuishi tena. Alisema, “Naam, mtu hutoa roho, anakufa, basi yuko wapi?” Akasema, “Wanawe wanakuja kumheshimu, wala hajui.” Kisha akasema, “Laiti ungenificha kaburini, kwamba ungeniweka mahali pa siri, hata ghadhabu Yako itakapopita. Umeniandikia muda na vifungo, nami siwezi kupita. Lakini laiti ungeniweka mahali pa siri mpaka siku ya ghadhabu Yako...”

⁴⁵ Papo hapo katikati ya dhiki yake, papo hapo wakati ikiwoko ile saa yenye giza kuu mno, katika wakati huo muhimu sana, ndipo akaja maskini Elihu na kuanza kuzungumza naye; akimwambia kwamba ua halikuwa limetenda dhambi; kwamba yeye ndiye aliyetenda dhambi, na kwamba kutakuwa na ufufuo. “Siku moja atakuja Mwenye Haki ambaye angekuja, akifananishwa na ulimwengu huu, na katika umbo la mfano wa Mungu, aliyeumbwa kwa mfano wa mwanadamu. Angejitwalia umbo la mwili wenye dhambi, vinginevyo, na angesimama kwenye pengo kati ya Mungu mwenye hasira, mtakatifu na mtu mwenye dhambi, na angeweza mikono Yake juu ya wote wawili na kuiunganisha njia.”

⁴⁶ Basi Ayubu alipoona hilo, alikuwa akiutazamia ufufuo wa Bwana. Akauona. Sasa angalieni. Kwa neno lingine, Ayubu alikuwa akijaribu kufikia hili, kwamba, “Ninajua ya kuwa mtu anapokwenda kwenye mavumbi ya nchi, yeye huchafuka tu na kwenda zake. Ninamwangalia. Hainuki tena. Anajilaza tu chini na kutoa roho, naye ameondoka. Basi yuko wapi? Hakuna ajuaye alipo. Lakini naona vitu vingine vikifufuka kutoka kwa wafu, lakini yeye hafufuki.”

47 Ndipo nabii huyu alipoingia katika Roho, Mungu alianza kumwonyesha yale yatakayotukia; ya kwamba kungekuwa na Mtu ambaye angeiondoa dhambi ya ulimwengu, na angefufuka tena. Aliona ufufuo wa Bwana. Halafu, ninapenda hilo, ninapowazia. Alisema alisimama. Akajitikisa.

48 Alikuwa ameketi kwenye lundo la majivu. Jamani! Kile tunachokiita, siku hizi, mkosi mbaya ulikuwa umeipiga nyumba yake. Watoto wake wote waliuawa. Utajiri wake wote ulikuwa umetoweka. Afya yake ilikuwa imezorota. Yeye ameketi, Mkristo, ama mwaminio, ameketi, aliyeachwa. Mtu, hata kanisa lake, lilikuwa limempa kisogo. Yeye ameketi pale, akiyakwangu majipu yake.

49 Ndipo Roho wa Bwana alipomjilia, naye akauona huu ufufuo asubuhi ya leo, mnajua, alisimama, akasema, “Najua Mkombozi wangu yu hai, na siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Na ingawa mabuu ya ngozi watauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu; Ambaye nitamwona mimi mwe- . . .” Alijua angemwona katika siku za mwisho, kwa sababu kutakuwa na ufufuo, ufufuo wa kiama.

50 Ninamwazia Daudi, alipokuwa anazeeka. Akiwa mfalme mkuu jinsi alivyokuwa, Mungu alikuwa amemwapia, kulingana na matunda ya viuno vyake angemwinua Kristo aketi mkono Wake wa kuume. Kisha namwona Daudi, alipokuwa mzee, akifikia mwisho wa safari yake, na nguvu zote za mwili zilikuwa karibu tu zimeisha. Akasema, “Tena, mwili wangu utakaa katika tumaini, kwa sababu hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu; wala hataiacha nafsi Yake katika kuzimu.” Alitangulia kumwona Yesu, ufufuo wa Kristo; na kujua ya kwamba mwili Wake haungekaa katika mavumbi ya nchi, bali ungefufuka tena.

51 Ninamwazia Ibrahimu kule nyuma wakati Mungu alipomketisha chini, na kusema, “Sasa, Ibrahimu, unazeeka, na umeupitisha ule umri, wewe na Sara nyote wawili. Lakini, umeupitisha umri wa kupata watoto, lakini nitakupa mwana wa ahadi.” Halafu jinsi Ibrahimu alivyosafiri akaingia katika nchi ya ahadi, na kungojea kule wakati ambapo huyu mbarikiwa angekuja, ambaye angemwakilisha Kristo Yesu.

52 Basi baada ya miaka ishirini na mitano ya kuamini ahadi hii, kabla tu ya ahadi kutimizwa, ndipo Mungu akamtokea Ibrahimu, na kumwonyesha ya kwamba, katika mauti, angemsulubisha Mwanawe; na, katika ufufuo, angemfufua tena, na angempa yote. Kufanya vivuli vishindwe, mambo yote ambayo yalikuwa yakimsumbua mwanadamu, na mauti, na vitisho vilivyokuwa katika mauti, vingeshindwa, watakapoona jambo hili.

53 Naye akampa mzee Ibrahimu onyesho lake la awali, Naye akapitia kwenye vipande hivi vya wanyama aliokuwa

amewakata-kata. Ambapo, ndio kwanza tulichukue majuma machache tu yaliyopita, ama juma lililopita, hasa, ama juma lililotangulia lililopita, katika ibada zetu; jinsi alivyoifanya Nuru hii ndogo nyeupe, ambayo ilikuwa ni Mungu, kupitia katika haya, akithibitisha kiapo cha agano.

⁵⁴ Ndipo akageuka na kumbariki Ibrahimu; akiwa mzee mwenye umri wa miaka mia moja, na mwanamke wa miaka tisini, akawageuza tena kuwa kijana mwanamume na kijana mwanamke, na wakamzaa mwa—mwana, Isaka. Ambaye, ndani yake, ulitokea Uzao wa Ibrahimu. Kutoka kwa Ibra-... Kutoka kwa huyo, kutoka kwa Isaka, akaja Daudi; kutoka kwa Daudi akaja Kristo; kutoka kwa Kristo ukaja ufufuo kutoka kwa wafu. Ni ahadi tukufu jinsi gani! Jinsi Mungu kote katika wakati alivyoonyesha awali mambo haya yote!

⁵⁵ Ndipo, hatimaye, na kama tulivyochukua katika siku chache zilizopita, kwa ajili ya msingi, jinsi ambavyo watu wote, manabii wote wa Agano la Kale, walivyotaja mahali pao pa kuzikwa.

⁵⁶ Leo hii utaenda makaburini, wengi wenu, mweke maua juu ya wapendwa wenu, au kwenye makaburi yao.

⁵⁷ Sasa angalieni hili. Manabii wote wa kale, bila kuwa na Maandiko yoyote ya kuendea, kama tulivyo nayo, ahadi yoyote ya Kiungu ya Mungu, kupitia tu kwa uongozi wa Roho Mtakatifu. “Watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliandika Neno la Mungu.” Kila mmoja wao, walipokufa, walitaja walitaka kuzikwa huko Palestina. Hawakutaka kuninii... Walikufia nje ya Palestina, wengi wao, lakini walitaka kuzikwa Palestina kwa sababu Mungu alitoa malimbuko ya ufufuo kutoka Palestina.

⁵⁸ Ndipo wakati Yesu alipokuja, basi walimfanyia yale waliyosema wangemfanyia. Alipozaliwa Bethlehemu, aliingia kwa njia ya mlango wa zizi, akatoka kwa njia ya adhabu ya kifo. Alipokuwa hapa duniani, Yeye kamwe hakufanya safari ya maili hamsini maishani Mwake. Hakwenda popote; kuizunguka Palestina, hata hivyo Ujumbe wa Injili Yake umesafiri katika kila ufa na kona ya ulimwengu.

⁵⁹ Hakuwahi kuandika kitabu maishani Mwake; hata hivyo kile Kitabu, kilichoandikwa juu Yake, kimeuzwa kuliko kila kitabu katika nyakati zote, Biblia. Na hata hivyo, humo ndani, kamwe Yeye hakupata kuwa na... Hakuwahi kwenda chuoni maishani Mwake, na hata hivyo kumekuwa na vyuo vingi vilivyojengwa kwa heshima Yake kuliko—kuliko kitu kingine chochote ambacho kimepata kuwako juu ya uso wa dunia, au jina lingine lolote au mtu mwingine yeyote. Naye hakuenda mbali sana. Aliishi maisha ya unyenyekevu, ya chini. Alitaniwa, alidhihakiwa, alichekwa.

⁶⁰ Naye alisema ya kwamba alikuwa na uwezo wa kuutoa uhai Wake, na uwezo wa kuutwaa. Mtu yeyote anaweza kujivunia

hivyo, mtu yeyote anaweza. Lakini Yeye alithibitisha madai Yake alipofufuka kwenye asubuhi ya Pasaka.

⁶¹ Wakati, walipoichoma mikono Yake, na miguu Ya—Yake, na ubavuni Mwake; na taji ya miiba juu ya kichwa Chake. Naye alikufa, kule, akilia apate rehema, pale Kalvari. Alipokuwa duniani, alionekana kama mwanadamu na alitenda kama mwanadamu. Na alipokufa pale Kalvari, alilia apate rehema, kama mwanadamu.

⁶² Lakini alipofufuka, asubuhi ya Pasaka, alithibitisha kwamba Yeye alikuwa zaidi ya mwanadamu. Alikuwa Mungu. Alikuwa na uwezo wa kuutoa uhai Wake.

⁶³ Sasa, jambo la kwanza, kwenye asubuhi hiyo, lile kundi dogo la wanafunzi wote walikuwa wamevunjika moyo. Hawakujua kilichokuwa kimetukia. Baadhi yao walitaka kurudi kwenye nyavu zao za kuvulia samaki.

⁶⁴ Sasa kama utangulizi mdogo wa kile mauti yalikuwa, na jinsi kifo kilivyokuwa cha kutisha, na kwa waanzilishi kote kupitia kwenye dini yetu ya Kikristo, jinsi ambavyo ahadi zilitolewa kupitia wazee hawa niliowataja asubuhi ya leo. Sasa hebu tushuke moja kwa moja hadi nyumbani, mahali ilipo.

⁶⁵ Maskini wanafunzi hawa, wakiisha...kundi dogo ambalo lilichukiwa hapo mwanzo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hawakuwa na marafiki wengi wa dunia hii.

⁶⁶ Na mtu yeyote anayemtumikia Yesu Kristo hatakuwa na marafiki wengi wa dunia hii. Huna budi kusimama juu ya imani yako, peke yako. Mara nyingi huna budi kusimama peke yako, lakini Yeye aliahidi angesimama pamoja nawe. “Nitaenda pamoja nanyi hata mwisho.”

⁶⁷ Na sasa, ninapomwona, hebu tuliangalie. Alikuwa amechukuliwa, walitarajia, kwa sababu angeweza kufanya miujiza. Naye alidai hakufanya lolote, kwa nafsi Yake, ila yale ambayo Baba alimwonyesha. Lakini Yeye—Yeye alikuwa mfanya miujiza. Na wakati alipotiwa mikononi mwa Pilato, wangewezaje kutarajia kumwona Masihi wa Mungu akivuliwa nguo, na mavazi Yake, na kusimama pale; na kupigwa, na kuchubuliwa, na kupondwa, na kugandamizwa, na kutemewa mate, wala hata asifunue kinywa Chake na kusema neno juu yake. Hilo lilikuwa limeivunja mioyo yao.

⁶⁸ Mtu yeye yule ambaye angeweza kunyoosha mkono Wake, na kusema, “Tulia,” nao pepo na mawimbi yakamtii.

⁶⁹ Yule ambaye angeweza kusimamisha msafara wa mazishi, na kuweka mkono Wake juu ya jeneza, na kusema, “Kijana, nakwambia, simama,” naye akatoka.

⁷⁰ Mtu ambaye aliingia katika nyumba iliyojaa huzuni, ambapo binti alikuwa amekufa hivi punde; Yairo, maskini kuhani mdogo ambaye angejiweka pamoja na Yesu, naye akawa

mwaminio. Naye akaingia ndani, akasema, “Tulieni, kwa maana huyo msichana hajafa; analala.” Hakika wangelijua. Hakika kulikuwa na kitu pale. Akaingia ndani, akamshika mkono; akamtazama, akasema, “Binti, nakwambia, simama.” Ndipo msichana aliyekuwa amekufa, na nafsi yake imeondoka, akasimama kwa miguu yake na akaishi tena.

⁷¹ Jinsi ambavyo alienda kwenye kaburi la Lazaro, akilia kama mwanadamu, machozi yakitiririka mashavuni Mwake, huku akilia na kusimama pale. Naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne, na mabuu ya ngozi wakitambaa kuingia na kutoka kwenye mwili wake. Lakini kumwona Yeye akiinua maskini mwili Wake namna *hiyo*, kasema, “Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe.” Wazieni hilo. “Yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe.”

⁷² Ni tumaini lililoje tulilo nalo asubuhi ya leo, basi, tunapozuru makaburi yetu, kwa mpendwa wetu! Ni tumaini la jinsi gani tulilo nalo katika mwili huu upatikanao na mauti, leo, huku Roho Mtakatifu akishuhudia, “Yu hai! ‘Hatakufa kamwe; yuna Uzima wa milele.’” Hata hivyo tunaibeba miili juu ya kaburi la aliye mtakatifu sana kati yetu, lakini ndani wako hai. Wanaishi mahali fulani.

⁷³ Aliposimama, alisema, “Mimi ndimi ufufuo na Uzima,” na palikuwa na mtu aliyelala pale. Akasema, “Liondoeni hili jiwe.” Na kuharibika kwa mwili wake, harufu hiyo ya mwili wa mwanadamu, mnajua ni nini. Walipouinua, mbona, walizungukwa na harufu mbaya pale. Lakini akanena, na kusema, “Lazaro, njoo huku!” Naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne, alifufuka kutoka kaburini.

⁷⁴ Wangewezaje kumwona Mtu mwenye nguvu za namna hiyo, akining’inia pale Kalvari, kwa dhihaka kuu, mafundo ya mate ya askari, waliomdhihaki, yakitiririka kutoka kwenye ndevu Zake; huku wakimng’oa makonzi ya ndevu usoni Mwake, na kumpiga kichwani, wakasema, “Tabiri useme ni nani aliyekupiga!” Walipoona misumari ya Kirumi ikipigiliwa mikononi Mwake na miguuni Mwake, wangewezaje kumwona Mtu kama huyo akifa? Kwa sababu, Mungu alihitaji hukumu, naye Kristo alichukua hukumu yetu.

⁷⁵ Jinsi walivyovunjika moyo sana! Walikuwa wamekwenda kwenye nyavu zao za kuvulia samaki tena. Petro alisema, “Ninaenda kuvua samaki.” Wanafunzi wakasema, “Nitaenda tu pamoja nawe.” Wakaenda. Kwa jumla walikuwa wamevunjika moyo kabisa, wamesikitishwa.

⁷⁶ Hapo wakaushusha mwili Wake, wakaufunga kwa kitani, na kuulaza kaburini.

⁷⁷ Wakasema, “Huo ndio mwisho wa mlokole huyo.” Jinsi ulimwengu ulivyomchukia! Wakasema, “Alikuwa mtakatifu

anayejibingirisha. Alikuwa mwendawazimu. Yeye alikuwa—Yeye alikuwa mlokole, na kadhalika.”

⁷⁸ Lakini Yeye alisema alikuwa Mungu. Alionekana kama Yeye. Alitenda kama Yeye. Alithibitisha alikuwa ni Mungu. Hiyo ni kweli.

⁷⁹ Mwanamke mmoja alisema, si muda mrefu uliopita, kama nilivyosema hili mara nyingi. Alisema, “Yeye hakuwa Mungu, Ndugu Branham.” Mwanamke wa Sayansi ya Kikristo, alisema, “Alikuwa mwanadamu tu.” Kasema, “Alikuwa mwanadamu tu.”

⁸⁰ Nikasema, “Alikuwa zaidi ya mwanadamu. Alikuwa Mungu.” Nikasema, “Ama alikuwa Mungu au mdanganyifu.”

⁸¹ Akasema, “Vema, kwa sababu alilia kwenye kaburi la Lazaro, Yeye alithibitisha ya kwamba hakuwa kitu ila mwanadamu.”

⁸² Nikasema, “Alipokuwa akilia, alilia kama mwanadamu. Lakini alipowafufua wafu, alithibitisha Yeye alikuwa Mungu.” Hiyo ni kweli. Nikasema, “Alipokuwa na njaa, aliona njaa kama mwanadamu.”

⁸³ Lakini mngeweza kuwazia mtu amesimama karibu na mtini, akijaribu kutafuta chakula; na siku chache baadaye, aokote biskuti chache, kama biskuti mbili, na vipande viwili au vitatu vya samaki, na kuwalisha watu elfu tano kwa samaki waliopikwa!

⁸⁴ Je, ungeweza kuwazia mtu amesimama pale Kalvari, akining’inia pale kati ya Mbingu na nchi, akilia, “Naona kiu, naona kiu”; na hata aliyageuza maji kuwa divai! Muumba mwenyewe wa—wa maji, amesimama pale, akilia apewe maji!

⁸⁵ Alifanyika dhambi kwa ajili yetu, ili sisi, katika umaskini—umaskini Wake tufanywe tajiri. Yeye, katika kifo Chake, alikufa kama mwenye dhambi; kusudi sisi, katika kifo chetu, tuweze kufa wana na binti za Mungu.

⁸⁶ Nawazia ni tofauti iliyoje kati ya vifo. Maskini Daddy Hayes hapa chini, alipokuwa akifa, aliwaita watoto wake kando ya kitanda. Na hapo, alikuwa katika hali ya kupoteza fahamu siku mbili au tatu. Alikuwa na msemu, akasema, “Mpendwa, naitakia heri roho yangu!” Alikuwa kabisa. . . Aliwaita watoto wake kando ya kitanda. Ndevu ndefu, nyeupe, zinazopepea; akasema, “Mpendwa, naitakia heri roho yangu! Mlidhani Daddy Haye amekufa.” Akasema, “Sitakufa kamwe. Kwa sababu Yesu yu hai, mimi pia ni hai.” Na hapo akambariki kila mmoja wa watoto wake.

⁸⁷ Kasema, “Inueni mikono yangu.” Asingeweza kuinua mikono yake. Ndipo mmoja wa wavulana wake akasimama upande mmoja, akainua mkono *huo*, huyo mwingine akainua mkono *huo*. Akaanza kuimba. Macho yake yalipoanza kutazama juu kuelekea Mbinguni, alisema, “Siku ya furaha, siku ya furaha,

tangu Yesu alipoosha dhambi zangu! Alinifundisha jinsi ya—ya kuomba na kuishi kwa furaha kila siku.” Ndipo akafumba macho yake, akaenda kukutana na Mungu. Nawaambia, hivyo ndivyo ninavyotaka kwenda. Hiyo ndiyo njia. Acha nife katika Yesu Kristo.

⁸⁸ Ndipo wanafunzi Wake walipokuwa wameona hayo, masikitiko yote na kila kitu, ambayo—ambayo—ambayo alikuwa nayo, ilionekana, alikuwa amewaaibisha. Wote wakaanza kurudi, wakavue samaki. Mmoja akarudi kazini mwake, na mwingine akarudi *huku*.

⁸⁹ Sasa, tunataka kuanza asubuhi ya leo kaburini. Kisha baada ya kufufuka Kwake, Mariamu, Martha, na yule Mariamu—yule Mariamu Magdalene, na Mariamu mama wa Yesu... Ilikuwa mapema asubuhi moja. Waliuweka mwili Wake ardhini, siku ya Sabato, ambayo ilikuwa ni desturi kwamba hawakufanya lolote siku ya Sabato. Kwa hiyo alikufa Ijumaa alasiri, saa tisa, akafufuka mapema Jumapili asubuhi.

⁹⁰ Sasa nataka kutatua swali hili, wakati mkiwa hapa asubuhi hii katika ibada hii ya mapambazuko. Watu wengi wanasema, “Imekuwaje basi kwamba Yeye alisema ya kwamba angelala... Alikuwa kaburini, siku tatu mchana na usiku?” Kamwe hakusema angefanya hivyo.

⁹¹ Alisema, “Katika siku hizi tatu nitaufufua mwili Wangu.” Mnaona? Sasa, sababu ya Yeye kufanya hivyo ni kwa sababu Daudi alikuwa amesema, mahali pamoja katika Maandiko, “Sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Naye alijua ya kwamba uharibifu huingia katika mwili wa mwanadamu baada ya saa sabini na mbili, siku tatu usiku na mchana. Na wakati fulani ndani ya hizo siku tatu mchana na usiku, Mungu alikuwa amfufue. Kwa hiyo alikufa Ijumaa alasiri saa tisa, na kufufuka mapema Jumapili asubuhi.

⁹² Sasa hebu tuchukue mchezo mdogo wa kuigiza papa hapa na tusimame kwa muda na kuangalia. Ninaweza kumwona, usiku kucha tu. Maskini Mariamu mkongwe, yule mama, moyo wake ulivunjika. Nabii mke Anna alimwambia angechomwa, ili kuyafunua mawazo ya wengi. Jinsi mwili Wake ulivyoteseka, na Mtoto wake mpendwa amening’inia msalabani, na ni fedheha iliyoje aliyokuwa ameiletea kanisa. Lakini hata hivyo, moyoni mwake, upendo huo wa mama ukajitokeza; kulikuwako... haidhuru Yeye alikuwa amefanya nini, ni fedheha jinsi gani. Alikufa, adhabu ya kifo, kama m—mfungwa leo ambaye angeenda huko nje, kunyongwa, ama kuuawa kwa umeme, ama chochote kile. Hivyo ndivyo alivyokufa, katika aibu na fedheha. Mnaona jinsi Mungu alivyoiadhibu dhambi? Na halafu jinsi alivyolia, labda usiku kucha! Naye na... .

⁹³ Mariamu Magdalene, alikuwa amejua nguvu Zake. Alijua kulikuwa na kitu juu Yake kilichokuwa tofauti na mtu mwingine yeyote. Alikuwa ametolewa pepo saba.

⁹⁴ Kila mtu ambaye amewahi kuwa huru na ibilisi, kwa nguvu za Yesu Kristo, anajua mahali wanaposimama. Hakuna mtu awezaye kuja, na katika Uwepo Wake mkuu wa Kiungu, na awe mtu yule yule tena. U—umebadilishwa. Kuna jambo linalokupata. Loo, unaweza kusimama mbali, na saikolojia, na kuwazia *hili*, na kukubali *hili*, jambo fulani, na nadharia fulani, au kitu kama hicho. Lakini hatuamini katika theolojia. Tunaamini katika nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo. Nawe unapokuja Mbele Zake, kuna jambo fulani linalotukia maishani mwako, ambalo linakubadilisha. Nawe si yeye yule tena, mtu aliyepata kuwa katika Uwepo wa Kristo.

⁹⁵ Kwa hiyo alitolewa pepo saba. Kiburi na wivu, naye alifikiri alikuwa mrembo sana wala hakukuwako na mwingine kama yeye. Lakini Yesu aliponena na kusema, “Takasika,” wote hao wakamwacha. Akawa mtu mpya. Hakuwa mrembo sana tena, machoni pake mwenyewe. Lakini alijivika vazi la upole na unyenyekevu, akamfuata Mwalimu. Alimpenda.

Kisha asubuhi ya Pasaka ninaweza kumwona.

⁹⁶ Wanafunzi wake walikuwa wametoka, wanavuta mashua za samaki; baadhi yao. Wengine wao wakienda nyumbani. Na wengine wakienda njia tofauti; warudi kwenye majukumu yao.

⁹⁷ Halafu mapema sana, ninaweza kumwona Mariamu mama, na Mariamu Magdalene, wakipanda kilima, kuenda kaburini. Walikuwa na baadhi ya manukato na kadhalika. Walitaka kuupaka mwili Wake mafuta na kumwacha.

⁹⁸ Na, kwa hiyo, huku wakipanda kile kilima, ninaweza kuwazia nikiona tukio lingine. Hebu tuangalie hapa.

⁹⁹ Ninaweza kuona kundi la askari wamesimama pale. Walikuwa wakicheza karata, usiku kucha, ama—ama kucheza dadu, au kucheza na dadu yao, da—da—dadu sakafuni. Na walikuwa wakipiga makelele. Baadhi yao wakisema, “Aisee, unamkumbuka yule mdanganyifu? Alisema ‘katika siku tatu’ atafufuka. Kwa hivyo sasa hebu tuone tu. Hebu twendeni kaburini.”

¹⁰⁰ Nami ninaweza kuwaona wakienda kule, na kujipigapiga kifuni mwao, na kutupa silaha zao kubwa namna *hiyo*, na upanga wa Kirumi; kasema, “Tutaona kile anachoweza kufanya!” Kwa sababu, kaburi lilikuwa limetiwa muhuri, muhuri wa Kirumi; ole wake avunjaye muhuri huo. Jiwe limewekwa pale, ambalo lilihitaji karne ya watu; yaani, watu mia moja walilifingirisha pale, jiwe kubwa mno walilolifingirisha kaburini. Kasema, “Yuko mle ndani, salama kabisa!” Na walikuwa na wakati mzuri sana.

¹⁰¹ Lakini wakija moja kwa moja, karibu na mapambazuko, Mariamu...huku wakipanda kilimani. Na kuna maskini wanawake wawili, wamewahi mapema, labda wamekumbatiana, wakienda zao. Loo! Loo, karibu naweza kuona hilo, jinsi walivyokuwa wakipitia kando ya kilima. Nami ninaweza kumsikia Mariamu, mama, akimwambia Mariamu Magdalene, "Aisee, ni nani atakayeliiondoa hilo jiwe kaburini? Ni kitu gani...? Tutafanyaje hilo?"

¹⁰² Vema, naweza kumsikia Mariamu akijibu, "Mungu atalishughulikia."

¹⁰³ Hilo ndilo jambo kuu. Haidhuru...Watu wanasema, "Je, nitafanyaje *hili* au *lile*?" Mungu atalishughulikia. Wewe endelea tu, unaona. Mungu atashughulikia mengine yote.

¹⁰⁴ Kisha, kwa ghafla, tunaona nyota zote zikianza kufifia. Na muda si muda mwajua, kuna nyota moja tu iliyosalia, hiyo ni ile nyota kubwa, angavu ya asubuhi iliyosimama kule.

¹⁰⁵ Ninaweza kuona jinsi kila kitu, na askari wakicheka na kufanya mizaha. Kasema, "Sasa, mnaona, kumepambazuka. Hakuna kilichotokea bado." Nao walikuwa wakiendelea, kasema, "Angalieni Yeye alikuwa tu ni mdanganyifu. Alikuwa ni mwanadamu tu kama wengi wa wadanganyifu walioinuka siku hizi, na siku zingine, na wamefanywa mambo haya, lakini basi...au wamefanya madai haya."

¹⁰⁶ Lakini basi, kwa ghafla, ninaweza kuwazia ndege wadogo wote, robini, wakiacha kuimba. Ndege wakaacha kuimba. Mshairi alisema, "Sauti Yake ni tamu sana hata ndege wananyamazisha kuimba kwao." Kitu fulani kilikuwa kinakaribia kutukia.

¹⁰⁷ Ninaweza kuona ile Nyota kuu ya Asubuhi ikining'inia kule kwenye tundu Lake, Yule aliyekuwa amening'inia huko tangu mwanzo wa wakati, ikianza kujongea. Ninaweza kuona ikizunguka. Mariamu, hao wengine, wakiitazama. Inafanya nini? Ni Malaika, Naye anatafuta kaburi walimomlaza. Maandiko yalikuwa tayari kutimizwa.

¹⁰⁸ Ndugu, dada, wakati wowote Maandiko ya Mungu yanapokuwa tayari kutimizwa, usijali, yatakuwa pale pale.

¹⁰⁹ Ninaweza kuona Nyota hiyo imeshika safari Yake, ikizungukazunguka. Ninaweza kuwaona Warumi wamesimama pale, mia moja wao, wenye nguvu, wakiwa wamechomoa panga zao, wakisema, "Sasa tutaona kitakachotendeka!"

¹¹⁰ Na, kwa ghafla, kimondo hiki kikubwa cha Moto kilichoruka kikaja kutoka Mbinguni, kikasimama kando ya kaburi. Basi kikatokea kuwa ni Malaika mkuu wa Mungu aliyesimama pale. Hao askari wakazimia na kuanguka chini kama watu waliokufa, ardhini. Kwa mtikiso tu wa mkono Wake, akalirudisha nyuma, lile jiwe lililokuwa limewekwa; akavunja muhuri wa Kirumi.

¹¹¹ Muhuri wa Kirumi unamaanisha nini Kwake? Si zaidi ya vile muhuri wa Marekani ungemaanisha, ama chochote kile, ama muhuri wa kanisa fulani, ama chochote kile. Mungu hana budi kuishi. Hana budi kutoka. Hawezi kuishi miongoni mwa wafu.

¹¹² Kwa hiyo analiondoa lile jiwe, nalo likafingirika nyuma. Naye akasimama pale. Sasa ni Nani anayechukua mamlaka? Askari wakinyakua ngao zao na kadhalika, na kukimbia upesi walivyoweza kukimbia, wakashuka kupitia bustanini, wakashuka kilimani; na kualika kwa nyenzo zao, chuma chao kilichokuwa juu yao, ngao zao na kadhalika.

Naye hapo amesimama, peke Yake. Baada ya muda kidogo, Mariamu akasema...

¹¹³ Kulikuwako na tetemeko kubwa la ardhi wakati hilo lilipotukia, ambalo liliitikisa ardhi yenyewe pale asubuhi hiyo. Mtu fulani anasema, "Sijui kama kitu kililipuka mahali fulani. Kulikuwa na... Lazima kulikuwako na m—mlipuko mahali fulani, wa radi, ama kitu fulani kiliipiga nchi." Lakini, jambo ni kwamba, Yesu alifufuka katika wafu.

¹¹⁴ Ndipo walipokwenda kaburini, Mariamu na Martha, walimwona Malaika amesimama pale. Akasema, "Nendeni mkawaambie wanafunzi Wake kwamba amewatangulia kwenda Galilaya, na huko atakutana nao. Tazama, nimewaambia. Nendeni upesi sasa, mkawaambie wanafunzi ya kwamba Yeye atakutana nao kama vile tu alivyosema angekutana nao."

¹¹⁵ Loo, ninapowazia hilo! "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua katika siku za mwisho."

¹¹⁶ "Tazama, nimewaambia." Malaika Wake wameeneza hilo kote ulimwenguni, kwamba, "Mtu yeyote ambaye angethubutu kujikana mwenyewe, na ajitwike msalaba wake na kumfuata, Yeye atakutana nanyi katika ufufuo." Inajalisha nini kama tukitapanya maua kaburini, kama tukisema "majivu kwa majivu, na mavumbi kwa mavumbi"? Mwili huo una hakika tu ya kufufuka kutoka kaburini kama vile kulivyo na Mungu Mbinguni. "Tazama, nimewaambia."

¹¹⁷ Hebu tuangalie. Hawa hapa wanaenda wawili wa wanafunzi Wake sasa. Wako safarini.

¹¹⁸ Na baadhi yao walikwenda kuvua samaki. Na kwa hiyo Yesu alikuwa amesimama ukingoni, Naye akaangalia nje, akawaona huko nje. Naye akasema, "Watoto, mna chakula chochote?"

¹¹⁹ Jambo la kwanza alilowaambia, alisema, "Twikeni wavu wenu upande huo mwingine." Walikuwa wamevua samaki usiku kucha, wasipate chochote. Hivyo ndivyo ilivyo; unavua samaki upande mbaya wa mashua. Basi Yesu akasema, "Twikeni wavu wenu upande huo mwingine."

¹²⁰ Ndipo wakatupa wavu wao upande wa pili, na kuvuta namna hiyo, jamani, kulikuwa na samaki wengi sana hata nyavu zao karibu kukatika.

¹²¹ Ndipo Petro akaanza kuangalia pande zote, akasema, “Kuna Mtu mmoja tu anayeweza kufanya hivyo.” Ndipo akatazama nyuma ukingoni, na huyo hapo amesimama; mkate na samaki juu ya moto, tayari kwa ajili yao. Petro asingeweza kusubiri mpaka mashua iingie. Aliruka tu majini, naye huyo akaenda, kukutana Naye. Ilibidi aharakishe.

¹²² Loo, laiti kila mwenye dhambi ulimwenguni angekuwa hivyo, leo. Petro alikuwa amemkana kule chini. Akatoka nje na kulia, kwa uchungu. Alikuwa ameomba kwa bidii. Alitaka kukutana na Yesu. Alitaka kushuka pale ili aanguke miguuni Pake.

¹²³ Kulikuwako na wawili jina lao, mmoja wa Kleopa, na kadhalika. Walikuwa wakienda zao Emau. Nao hao hapo wanaenda zao, wenye mioyo mizito, iliyovunjika. Nao walikuwa wakienda zao, wakilizungumzia, loo, jinsi ilivyokuwa mbaya. Na kwa ghafla, Mtu fulani akatokea vichakani; Mtu wa kawaida, si mwenye ukosi uliopinduliwa, ama kuvalia vinginevyo.

¹²⁴ Alivaa kama watu wengine wote. Aliweka nywele Zake na ndevu Zake kama tu hao wengine walivyofanya. Hakuninii... Hakuwa tofauti hata kidogo. Hakufanya tofauti yoyote kubwa. Maisha Yake yalithibitisha sifa Zake, kile alichokuwa. Na hivyo ndivyo Mungu anavyotaka tuwe; anataka maisha yetu yawe sifa zetu. Hiyo ni kweli.

¹²⁵ Na ndipo akaanza kutembea pamoja. Akasema, “Ndugu, mbona mna huzuni hivi? Na kwa nini mko kwenye mazungumzo haya?” Loo, ninapenda tu hilo!

¹²⁶ “Mbona,” walisema, “Kwani wewe ni mgeni hapa, Bwana? Mbona,” akasema, “nchi nzima imevurugika. Na sisi hapa,” akasema, “tuko njiani, tunarudi nyumbani.” Akasema, “Mbona, Yesu wa Nazareti, yule Nabii, tuliyedhani hakika kwamba angeninii, atakapokuja, kwamba angekuwa Mfalme wa Israeli. Na sasa amekufa, nao wamemzika. Nao walimchoma moyoni. Na wamemwondosha.” Kisha kasema, “Hata hii ni siku ya tatu tangu yote yalipotendeka, tangu alipouawa.” Kisha kasema, “Baadhi ya wanawake walikuwa kule chini kaburini na—nao wakaona ono la Malaika, kisha wakarudi na kusema Yeye alikuwa hai. Lakini,” kasema, “loo, tusingeweza kuamini hadithi hiyo. Tunaendelea tu.”

¹²⁷ Kwa hiyo wakienda zao pale, Yeye alisema, “Enyi msiofahamu, na wenye mioyo mizito, mnaona, kutokuamini yote waliyosema manabii katika habari za Kristo, jinsi impasavyo kupata mateso, na kufufuka siku ya tatu. Vema, jinsi mliyvo wavivu!”

¹²⁸ Angalieni jinsi lilivyo zuri! Jamani! Angalieni hili, Kristo miongoni mwa wenye huzuni na waliovunjika moyo! Hapo ndipo aendapo, miongoni mwa wale wenye huzuni na waliovunjika moyo.

¹²⁹ Walikuwa wakienda zao katika saa yenye giza sana waliyopata kuona. Matumaini yao yote yalikuwa yamekwisha. Walikuwa wamefukuzwa kanisani, masinagogi, kwa sababu walimwamini. Na sasa Yeye, Yule waliyekuwa wamemwamini, alikuwa amekufa. Na baadhi ya wanawake walikuwa wamekuja na hadithi ndogo kuhusu ono fulani, walikuwa wamewaona Malaika, “Waambieni Wanafunzi Wake atakutana nao Galilaya.” Lakini, loo, alininii tu... Wasingeweza kuamini hilo. Walikuwa wamevunjika moyo na kuhuzunika, wakilia. Na hapo Yesu mpendwa akatokea, miongoni mwa waliovunjika mioyo.

¹³⁰ Jambo lingine, ilikuwa asubuhi ya kwanza ya Pasaka. Yesu, ufufuo wa uhai wote, alikuwa hai na katikati ya majira ya kuchipua, katikati ya kuimba kwa ndege, katikati ya kuchipusha kwa maua mapya. Yesu aliyefufuka alikuwa katika majira ya kuchipua, pia, kutokea kwa u—ufufuo.

¹³¹ Jinsi ambavyo alitembea pale pamoja nao, na kuanza kuzungumza nao, akiwaambia. Kasema, “Vema, sasa, mnapaswa kuamini yale manabii waliyosema. Mnapaswa kuamini, kile Maandiko yote yaliyoandikwa, kuhusu Kristo; jinsi inavyompasa kupata mateso, na kufufuka tena siku ya tatu, na kadhalika.” Vema, walikuwa wamevunjika moyo kupita kiasi.

¹³² Baada ya kitambo kidogo, baada ya Yeye kuanza kunena, kulikuwa na kitu kuhusu Mtu huyu ambacho kilizungumza tofauti kidogo na watu wengine. Hakuwa mtu wa kawaida. Kulikuwa na kitu fulani kumhusu ambacho kilionekana kuwa na ukweli mtupu. Kulikuwa na kitu fulani kuhusu hilo kilichokuwa na maana, Naye akaanza kuyaelezea Maandiko. Alikuwa Mwalimu wa Maandiko; jinsi manabii walivyosema ya kwamba Kristo angekufa, na kufufuka tena siku ya tatu. Jinsi mioyo yao ilivyoanza kuwaka ndani yao! Jambo fulani lilikuwa linatukia.

¹³³ Nao walipokuwa wakisafiri, walizungumza mchana kutwa. Sasa walikuwa umbali wa maili chache, yapata maili moja na nusu, kutoka Yerusalemu, walikokuwa wanaenda. Wakitembea polepole, pamoja na Kristo aliyefufuka, wala hawakujua.

¹³⁴ Ni mara ngapi ameketi kitini pamoja nawe! Ni mara ngapi amesimama pamoja nawe katika saa za majaribu yako na shida zako, wala hukutambua! Ni mara ngapi alipokuwa usukani wakati nusura uuawe katika ajali hiyo, ama ukakwepa tu ajali hiyo ama chochote kile, wala hukutambua ilikuwa ni Yeye! Jinsi ambavyo alikuwa pamoja nawe wakati pipa lilipokuwa tupu, na chupa ikakwisha, wala hapakuwapo na kitu kwa ajili ya watoto

wachanga; jinsi ambavyo mtu huyo alikuja na kuweka vyakula hivyo mlangoni, chochote kile! Huyo alikuwa ni Kristo. Yu hai leo. Hajafa, bali Yu hai.

¹³⁵ Nikiwa nimesimama asubuhi chache zilizopita, karibu na daktari kafiri sana, kule Louisville. Alikuwa . . . Nilikuwa huko chini, baada ya kurudi kutoka Afrika. Walikuwa wakinifanyia uchunguzi wa amiba. Akasema, “Kasisi Branham,” akasema, “na unaamini huo ni ujinga . . .?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

¹³⁶ Naye akasema, “Unataka kuniambia unaamini kuwa Mtu huyo alifufuka katika wafu?”

Nikasema, “Naam, bwana, ninaamini.”

¹³⁷ Naye akasema, “Unawezaje kuthibitisha kwamba alifufuka katika wafu?”

Nikasema, “Ninaweza kuthibitisha kwamba Yeye ndiye Kristo aliyefufuka.”

“Anawezaje?”

¹³⁸ Nikasema, “Anaishi moyoni mwangu. Hivyo ndivyo ninavyojua alifufuka. *Hapa* ndani, alinibadilisha kutoka mwenye dhambi nikawa Mkristo. Alibadilisha asili yangu. Alibadilisha mitazamo yangu. Alibadilisha yote yaliyokuwa ndani yangu. Alinifanya kiumbe kipya. Kwa hiyo ninajua, binafsi, kwamba alifufuka katika wafu.”

Akasema, “Ninaamini alikufa.”

¹³⁹ Ni—nikasema, “Ninaamini, pia. Lakini, alikufa. Naam, zaidi ya hayo, alifufuka katika wafu.”

¹⁴⁰ Na leo hii anaishi ndani ya mioyo yetu. Hiyo ndiyo sababu tuna furaha na tunaweza kuimba. Hiyo ndiyo sababu tunaweza kumwona. Hapa si muda mrefu uliopita, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alinifanyia mwujiza mkuu katika maisha yangu mwenyewe. Amefanya miujiza kwa ajili yako. Anatembea pamoja nawe kila siku. Anatembea na kila mwaminio. “Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.” Haijalishi kijacho wala kiendacho, Kristo angali hai na anatawala siku hizi katika moyo wa mwanadamu.

¹⁴¹ Hiyo ndiyo sababu, kama hadithi ilivyosema; hebu angalieni, kila asubuhi, tunaamka tukinung’unika, na kutoka nje, na, “Vema, karibu nimelala nusu,” na kadhalika. Si ajabu tuna shinikizo kuu la damu, na kisukari, na kila kitu kingine.

¹⁴² Mwangalie maskini robini. Ataamka, kila asubuhi, jambo la kwanza, ataurusha uso wake mdogo juu mbinguni na kuanza kuimba kwa sauti yake yote. Hujawahi kuona yeyote kati yao mwenye shinikizo kuu la damu, akitembea kwa magongo, akiwa na kisukari.

¹⁴³ Kasema, maskini robini alisema, wakati mmoja, alisema, “Vema, sijui kuna shida gani,” kasema “watu hawa, mambo haya, na viumbe wanaojiita wanadamu?” Kasema, “Mbona, hapana shaka wana huzuni sana. Labda hawana Baba wa Mbinguni kama sisi tulivyo naye, anayetushughulikia.”

¹⁴⁴ Usiku mmoja, nikifanya mkutano hapa katika kanisa la Kibaptisti la Milltown, nilipokuwa mchungaji kule chini. Nilikuwa nikirudi nyumbani na rafiki yangu wa zamani, kukesha usiku kucha. Nami nilikuwa nikiona, nilipokuwa nikipita, kungekuwako na kinega ameketi kwenye kichaka cha mwerezi pale. Usiku kucha angeimba kwa sauti yake yote, kwa sauti kubwa kadiri alivyoweza kuimba. Jinsi ningeweza kuelewa vizuri ni kwa nini ndege huimba kunapopambazuka. Ninaweza kuwazia mwanga wa jua ukiwaogesha, unawafanya waimbe. Lakini ni kitu gani kinachomfanya kinega huyo aimbe?

¹⁴⁵ Kwa hiyo nikachukua kitabu na kuanza kusoma juu ya kinega. Nikagundua ya kwamba, kinega, kinachomfanya aimbe, ni kwamba yeye huangalia anga. Na kila wakati anapoweza kuangalia kuona mawingu yakianza kurudi nyuma, na kuona nyota moja, mwali mmoja wa nuru, anaanza kupiga kelele na kuimba kwa sauti yake yote. Kwa nini? Kwa sababu anajua jua linawaka mahali fulani. Anaiambia dunia tena kwamba jua linawaka mahali fulani.

¹⁴⁶ Basi, ndugu, dada, maadamu chini moyoni mwangu, kupitia mawingu meusi ya mateso, na majaribu na shida, kama ninaweza kumhisi Roho Mtakatifu akipenya mara kwa mara, na kunipa baraka, ninajua Nguvu za Mungu zingali hai na zinatawala mahali fulani. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁷ Kama ningeweza kuiuliza nyota hiyo ya asubuhi, “Ni nini kinachokufanya uangaze huko juu? Kwa nini unaangaza?”

¹⁴⁸ Angeweza kusema, “Si mimi ninayeangaza, Ndugu Branham,” ikiwa hiyo nyota ingeweza kunena. “Ni jua tu likinimulikia, ambalo linanifanya niangaze.”

¹⁴⁹ Na hivyo ndivyo ilivyo kwa kila mtu ambaye ni mwaminio wa Yesu Kristo, ambaye amefichwa ndani Yake. Si wewe unayeangaza, ni Roho Mtakatifu anayekuangazia, anayekupa tumaini hili na furaha hii ya ufufuo.

¹⁵⁰ Nilikuwa nikisema juu ya, nikizungumza hapa chini, kuhusu chemchemi ya kale niliyozoea kuinywea. Ilikuwa ikibubujika na kuruka, na kuruka na kuruka, huko chini karibu na Milltown. Nilikuwa nikishangaa ni kwa nini chemchemi hiyo iliruka, kwa hiyo siku moja niliketi pale chini nami nilikuwa nikizungumza nayo. Waweza kuwazia mtu akizungumza na chemchemi? Lakini nilikuwa nikizungumza na Asili Yule aliyeiumba hiyo chemchemi. Nami nikashangaa, “Ni nini kinachokufanya ububujike hivi, mwenye kurukaruka hivi? Ni

kwa sababu ati—ati watoto huja hapa na kunywa kwako, ama mimi hunywa kwako, ama chochote kile?”

¹⁵¹ Kama hiyo chemchemi ingeweza kujibu, ingesema, “La, Billy, si kwa sababu unakunywa humo. Si kwa sababu mtu yeyote anakunywa kwangu. Ni kitu fulani chini yangu hapa, kinachonisukuma na kunifanya nibubujike na kuruka-ruka, na kupiga makelele hivi.”

¹⁵² Hivyo ndivyo, kila mwanamume ama mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu. Si wewe. Sio mhemko wa kibinadamu. Ni kwa sababu ufufuo, ama Nguvu za Mungu, zimo katika maisha hayo ya mwanadamu, nazo zinasukuma juu kuingia katika Uzima wa Milele, kuingia katika Uzima wa Milele. Kitu fulani humu ndani! Usingeweza kunyamaza hata ufanye nini. Kuna kitu fulani ndani yako.

¹⁵³ Yesu alipokuja, akitembea kuingia Yerusalemu, nao wakakata mitende na kuanza kupiga mayowe na kulia na kuendelea namna hiyo. Baadhi ya hao Mafarisayo wagumu walisema, “Wafanye wanyamaze. Mbona, wanatuogofya. Loo, jinsi hao watu wanavyopiga makelele na mayowe!”

¹⁵⁴ Akasema, “Wakinyamaza, miamba italia mara moja.” Kitu fulani hakina budi kuja. Uzima unapokuja miongoni mwa mauti, kuna ufufuo; hapana shaka.

¹⁵⁵ Na wakati Uzima ulio ndani ya Yesu Kristo utakapokuja kwenye makaburi ambapo wapendwa wetu wamelala, kutakuwako na ufufuo. Uzima na mauti haviwezi kukaa pamoja si zaidi ya vile giza na mwanga wa mchana vinavyoweza kukaa pamoja. Mara tu giza. . .

¹⁵⁶ Mara tu mwanga wa mchana ujapo, husukumia giza mbali. Mwanga wa mchana hauna budi kuangaza. Haijalishi kinachotendeka, wakati ulimwengu huo unapozunguka huko, mbele ya jua hilo, hapana budi kupambazuke. Hapana budi.

¹⁵⁷ Na kwa hakika tu kama Umilele, unapojivutia kwenye wakati wa kuja kwa Mwana wa Mungu, kutakuwako na ufufuo juu ya ulimwengu huu. Na wote waliolala katika Mungu, Kristo atawaleta pamoja Naye katika kufufuka Kwake. Itabidi iwe. Hakuna njia ya kuliepuka. Huna budi kuwa nao. Na unawezaje kuwa nao isipokuwa uwe *hapa* ndani?

¹⁵⁸ Nikiwa nimesimama siku moja, nilikuwa nimesimama huko Gary, Indiana, ambapo walinitembeza kwenye viwanda vikubwa vya Gary steel. Na nilishangaa sana, nilipokuwa nikitazama. Msimamizi alinipandisha juu, na alikuwa akinionyesha kila mahali. Naye akasema. . . Nilikuwa nikiwaangalia watu.

Filimbi ndogo ikapigwa, dakika tano kabla ya wakati wa kuondoka. Niliona kila mtu akivua aproni yake na kuiweka juu ya mashine yake. Na moja kwa moja kupitia, karibu na kerezo zake na kadhalika, alikuwa akifagia kwenye marefu, lundo la

takataka ambazo zilikuwa zimekusanywa kutoka kwa nyenzo alizokuwa akifanyia kazi. Naye akazifagia zote nje kwenye hayo marefu. Naye akasema, “Nitakuonyesha jambo fulani hapa, Kasisi Branham.”

Nikasema, “Sawa.”

¹⁵⁹ Ndipo, akarudi nyuma mahali padogo. Baada ya filimbi kuu kupigwa, watu wote wakatoka nje. Kila mtu alikuwa ameondoka humo jengoni; tukabaki tumesimama peke yetu. Ndipo akabonyeza kitufe. Na huko nyuma kabisa, nikasikia kitu kikinguruma, na kunguruma, na “bruu,” kikishuka chini. Nikawazia, “Ni kitu gani hicho?”

¹⁶⁰ Baada ya kitambo kidogo, akasema, “Sasa wewe simama kando.” Nikasimama kando.

¹⁶¹ Nikaona mtambo ukishuka kupitia hapo. Na uliposhuka, hii hapa sumaku kubwa ikishuka kupitia pale. Basi wakati sumaku hiyo ilipopitia kwenye mstari huo, nikaanza kuona takataka hizo zikiruka juu kukutana nayo, namna hiyo, hizo takataka za chuma. Nikaona baadhi yake hazikupanda juu. Nami nikaona vipande kadhaa vya chuma havikupanda juu. Ndipo sumaku hiyo ikarudi tena ndani ya kuba na kuye-...ikatupa vitu hivi vyote kwenye hiyo kuba, nazo zikayeyuka na kutengenezwa upya.

¹⁶² Ndipo nikasema, “Vema, kwa nini hazikuinuka zote?” Nikasema, “Ninaona baadhi ya takataka.”

¹⁶³ Akasema, “Kasisi Branham, tunatengeneza sehemu za alumini hapa.” Akasema, “Na vipande hivyo vya alumini havijatiwa sumaku ya sumaku ile.”

Nikasema, “Bwana asifiwe!” Kisha—kisha nikasema . . .

Akasema, “Kwani una shida gani?”

¹⁶⁴ Nikasema, “Nilikuwa nikiwazia tu.” Kwa hiyo nikasema, “Kwa nini—kwa nini hivyo vipande vingine vya chuma havikupanda juu?”

¹⁶⁵ Kasema, “Kama uliangalia, vimefungiwa chini. Haviwezi kupanda juu.”

Nikasema, “Mungu asifiwe! Haleluya!”

Akasema, “Kuna nini, Kasisi Branham?”

Nikasema, “Nilikuwa nikiwaza tu.”

Alisema, “Hapana shaka ulikuwa unawaza.”

¹⁶⁶ Nikasema, “Ndugu, huko nyuma sana mahali fulani, katika Umilele, haleluya, kuna sumaku kubwa. Mwana wa Mungu atafunguliwa, moja ya asubuhi hizi. Anaenda kote katika dunia hii, kama sumaku. Na kila mtu aliyetiwa sumaku Yake atapanda kwenda kumlaki hewani, na awe huko katika ule ufufuo, kuishi pamoja Naye, kupandishwa huko juu. Na miili hii ya kale tunamoishi sasa, ama hata kama tuliyo nayo sasa, ambayo

inazeeka, na kukunjamana, na kushuka chini; itamwagwa kule kwenye kuba ya udongo, na kufinyangwa upya, na kufanywa kama mwili Wake Mwenyewe wa utukufu, katika ufufuo wa mwisho, atakapokuja tena.”

¹⁶⁷ Nami nikasema, “Vema, sasa angalia hapa, kuna watu wengi ambao hawajatiwa sumaku. Kuna watu wengi ambao wamefungiwa chini na hali ya mambo, wanasema, ‘Siwezi kulifanya. Kamwe nisingeweza kulifanya. Ni gharama kubwa mno.’”

¹⁶⁸ Ndugu, isipokuwa moyo huo ubadilishwe, na hiyo nafsi inayokaa mle, itiwe sumaku na Mungu kwa Roho Mtakatifu, Yesu atakapokuja, utaachwa peke yako duniani. Kumbuka, kutakuwa na ufufuo moja ya asubuhi hizi, kwa wale tu waliokufa katika Kristo, Mungu atawaleta pamoja Naye.

¹⁶⁹ “Akitembea miongoni mwa wanafunzi, akijitambulisha Mwenyewe,” tuseme, “akijitambulisha Mwenyewe.”

¹⁷⁰ Ninao watu, kila mahali nchini kote, wakati mwingine wakinishutumu kuhusu uponyaji wa Kiungu. Mbona, ndugu yangu, ningewezaje kujizuia kuamini katika uponyaji wa Kiungu, wakati ndiyo asili yenyewe ya Roho Mtakatifu. Kila mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu itambidi kuamini katika mambo ya kimbinguni, kwa sababu yeye ni sehemu ya Mungu, yeye ni mtoto wa Mungu.

¹⁷¹ Nasema, “Unafanana na baba yako.” Aisee, “Una pua kama . . .” Wananiambia nina pua kama ya baba; nina kinywa kama cha baba. Kwa nini? Yeye ni baba yangu. Nina haki ya kufanana naye.

¹⁷² Haleluya! Basi, kama Mungu ni Baba yangu, nina haki ya kuamini katika mambo ya kimbinguni, kwa sababu nimezaliwa kwa Roho wa kimbinguni. Hiyo inanifanya kiumbe cha kimbinguni. Kwa ndani, kwa nje, mimi ni—mimi ni mtu wa udongo; wewe ni mtu wa udongo. Lakini kwa ndani, unapozaliwa kwa Roho wa Mungu, unakuwa kiumbe cha kimbinguni humo ndani, nacho hicho kiumbe cha kimbinguni kinaona njaa na kiu kwa ajili ya Makao yake ya Mbinguni, huko ng’ambo. Hiyo ni kweli. Amina. Liangalie.

¹⁷³ Hao hapo. Huyu hapa anatembea sasa. Amefufuka katika wafu. Furaha inaanza kuja. Wanafunzi wanaanza kupata mruko zaidi kidogo katika hatua yao. Jambo fulani limetendeka; amefufuka katika wafu.

¹⁷⁴ Hivyo ndivyo ilivyo kwa kila mwanaume au mwanamke, anapozaliwa kwa Roho wa Mungu, na kuona ufufuo wa kweli. Hakuna mtu ajuaye ya kuwa Yesu amefufuka katika wafu, isipokuwa amekufa, yeye mwenyewe, katika Kristo Yesu, na kuzaliwa mara ya pili, upya na Roho Mtakatifu. Kila mtu anaamini tu kitheolojia, anaamini tu kinyenzo, anaiangalia tu kwenye karatasi, mpaka Roho Mtakatifu ametoa ushuhuda wa

kufufuka kwa Yesu Kristo. Wewe, kutoka kwa vitu vilivyokufa vya maisha, hadi kwenye tumaini jipya na lililo hai katika Kristo Yesu. Kila mwanamume au mwanamke asiye na hilo amepotea, asubuhi ya leo. Hiyo ni kweli.

¹⁷⁵ Loo, ndugu yangu, dada, kuwa sawa na Mungu. Safisha moyo huo, kufikia ambapo kengele za furaha za Mbinguni zinalia, na kuna ufufuo; Yesu anaishi na kutawala moyoni.

¹⁷⁶ Angalia wanapoanza kwenda kando ya barabara. Nafikiri hilo lilikuwa jambo la ajabu sana pale. Nayo Biblia ilisema ya kwamba waliendelea, barabarani, na wakasemezana wao kwa wao. Nao walipofika mwisho, mahali tu ambapo walikuwa wanaenda kukaa usiku kucha, kamwe hawakutaka Yeye aondoke.

¹⁷⁷ Kuna jambo fulani tu kumhusu, kama ukipata tu kufahamiana Naye, hutaki aondoke. Hiyo ni kweli. Sasa Yeye...

Walisema, "Ingia ndani ukae nasi."

¹⁷⁸ Napenda hilo, "Ingia ndani ukae." Kila mtu ambaye amewahi kukutana na Yesu Kristo anataka Yeye akae. "Kaa nasi." Ulimwengu umekufa. Kristo amefufuka. Yeye Huyu hapa, akiishi pamoja nasi. Vema.

¹⁷⁹ "Ingia ndani ukae pamoja nasi. Inakaribia..." Basi, Yesu, sasa kumbukeni, walimkaribisha ndani.

¹⁸⁰ Na kila mtu amjiaye Kristo itamlazimu kumwalika Kristo katika nyumba yako ndogo unamoishi. Yeye huja tu kwa mwaliko. Hajisukumizi Mwenyewe kwako. Unasema, "Sitaki upuuzi wowote huo wa kilokole," sawa, usijali, hautakuwepo. Lakini wakati unataka na uko tayari, na uko tayari kuachana kabisa na mambo ya ulimwengu!

¹⁸¹ Kama vile nilivyozungumza jana usiku na wamishenari. Nilisema, "Naam, unaenda hapa shuleni na kujifunza theolojia yako, na unatoka hapa nje, kusoma, kuandika, na hisabiti; kisha unaenda Afrika na kufanya mtoto maradufu zaidi, wa kuzimu, kutoka kwa hao wenyeji, kuliko ulivyofanya hapo kwanza."

¹⁸² Lakini nikasema, "Yesu, alipowaagiza wanafunzi Wake waende kuwa wamishenari, Yeye alisema, 'Angalieni, nawaletae juu yenu ahadi ya Baba, lakini ngojeni kwanza katika mji wa Yerusalemu,' sio katika seminari fulani, sio katika shule fulani ya elimuadili. Alisema, 'Ngojeni katika mji wa Yerusalemu mpaka mvikwe Nguvu zitokazo Juu. Tazama, nawaletae juu yenu ahadi ya Baba, bali ngojeni katika mji wa Yerusalemu, hata mvikwe Nguvu zitokazo Juu. Huyu Roho Mtakatifu akiisha kuja juu yenu, ndipo mtakuwa wamishenari, au mashahidi, kwangu katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na hata pande za mwisho za dunia.'"

183 Na mpaka mtu amejazwa na Roho Mtakatifu; si kwa elimu, si kwa theolojia, si kwa ufuasi wa kanisa! Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . amekuwa Yerusalemu na kujazwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, hastahili kuwa mimbarani, hiyo ni kweli, kama mmishenari ama chochote kile.

184 Na wakati Filipo aliposhuka kwenda kule, mmishenari wa kwanza aliyepata kutoka nje, aliposhuka kwenda Samaria. Basi alipofika kule chini, alihubiri Injili, akawaponya wagonjwa, na kuyafungua macho ya vipofu, akayafungua masikio ya viziwi. Kulikuwa na furaha kuu mjini.

185 Na kila mahali mmishenari wa kweli wa Mungu, au mhubiri aendapo, kuna kengele za furaha zinazolia, za ufufuo wa Kristo. Huwezi kuweka mauti na Uzima pamoja; zitatengana. Amina. Ndipo Kristo anapoingia katika moyo wa mwanadamu, Yeye hukutenga na vitu vilivyokufa vya ulimwengu, ukaingia katika tumaini lililo hai, na kuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu, naye anakuwa mtu mpya. Ninawaambia, ndugu zangu, kama ulimwengu unahitaji kitu chochote leo, ni kuhubiriwa ufufuo halisi, wa kweli wa Kristo.

186 Wanasema, “Njoo ukae pamoja nasi. Jioni, mchana unakwisha. Vema, tuliwasikia hao wanawake, walichosema, tunashangaa kama yote ni kweli vya kutosha?” Wakienda zao, kidogo wakiwazia juu ya kitu kingine. Lakini akasema, “Karibu sasa, kwa muda kidogo tu.” Wakasema, “Karibu sasa ukae pamoja nasi.” Alifanya kama anataka kuendelea mbele. Mara nyingi Yeye hufanya hivyo, apate tu kuona kile utakachofanya. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo baada, baada ya kitambo kidogo, wakamsihi. Wakasema, “Karibu ndani.”

187 Wakaingia, labda wakachukua menyu, wakasema, “Sasa utakula chakula gani cha jioni?”

188 Na wakaanza, wakasema, “Kaa pamoja nasi. Tunakupenda Wewe sana. Mbona, tungependa kukuchukua kama mchungaji wetu. Kuna kitu kukuhusu Wewe ambacho ni tofauti na watu wengine. Kuna kitu fulani kukuhusu Wewe; unayaelezea Maandiko tofauti kidogo na watu wengine. Tungependa tu Wewe u—uende pamoja nasi. Tungependa ukutane na rafiki yetu, Petro, Yakobo, na Yohana, na hao wengine. Tuna marafiki kadhaa waliokuwa mfuasi wa Yesu, nasi tungependa Wewe uingie. Inaonekana kana kwamba unajua mengi sana juu Yake.” Na ilikuwa ni Yeye, Mwenyewe. Huyu alikuwa ni Yeye. Ameketi karibu nawe mara nyingi.

189 Hapa Yeye amesimama pale, Naye akaanza kuzungumza nao. Na kwa hiyo, muda si muda mwajua, wakati alipoutwaa ule mkate. . . Aliutwaa mkate. Sasa, macho yao yalipofushwa. Naye akaumega mkate. Alipoinua macho Yake, na kuubariki na kuuvunja, ndipo macho yao yakafumbuliwa. Napenda hilo. Macho yao yakafumbuliwa. Kama kuliwahi kuwa na wakati

ambapo kanisa la Kristo linahitaji kufumbuliwa macho yake, ni leo hii; kumegwa tena kwa mkate. Macho yao yalifumbuliwa nao wakamtambua kuwa Ndiye.

¹⁹⁰ Loo, rafiki, je, Yeye amewahi kuyafumbua macho yako namna hiyo? Je, amewahi kukubariki namna hiyo? Je, amewahi kukutenga na mambo ya ulimwengu, akakutenga, wakati wa kuvunja na wa kufungua. Hicho ndicho kanisa linahitaji leo hii, ni wakati wa kuvunja na wa kufungua. Na macho yake yakafumbuliwa, macho yao yakafumbuliwa, hasa, nao wakamtambua. Jinsi tu alivyofanya mkate ule, hivyo ndivyo walivyomtambua. Jamani, ni mara ngapi. . .

¹⁹¹ Hapa si muda mrefu uliopita, mama mmoja alikuwa chini hapa pembeni. Alikuwa na TB. Nadhani ameketi kanisani asubuhi ya leo. Siwezi kulikumbuka jina la huyo mwanamke. Anaishi ng'ambo. . . Reese. Asante, dada. Hiyo ni kweli. Bibi Reese, alikuwa amelala pale, alikuwa na watoto watatu ama wanne, nami nikashuka kwenda kumwombea. Alikuwa ametumwa kutoka kwenye hospitali hapa juu, apate kufa. Na kwa hiyo nikashuka kwenda kumwombea.

¹⁹² Basi kulikuwa na kafiri jirani yangu, naye alifanya kazi hapa serikalini, Bw. Andrews. Kwa hiyo nilikuwa nikipita kona, kwa maskini baiskeli yangu. Na—nami nilikuwa nimemwombea mwanamke huyo, usiku, siku kadhaa usiku kabla ya hapo. Nikaenda nyumbani. Nilipokuwa nimeketi barazani, Bwana alinionesha ono ya kwamba mwanamke huyo angeishi.

¹⁹³ Kwa hiyo, nikashuka kule. Nikasema, “Nina BWANA ASEMA HIVI, kwa ajili yako. Utaishi.”

Naye akasema, “Loo, Mungu ashukuriwe,” maskini mama huyo.

¹⁹⁴ Nikasema, “Je, utasimama na kubatizwa katika Jina la Bwana, ukimwitia Yeye, na kuoshwa dhambi yako?”

¹⁹⁵ Akasema, “Nitafanya chochote ambacho Mungu ananiagiza kufanya. Njoo tu na unielekeze, na uniambie, nami ninitalifanya.”

Nikasema, “Vema.”

¹⁹⁶ Asubuhi kadhaa baada ya hapo, nikakutana na m—mtu akishuka mtaani kule, na ilikuwa ni Bw. Andrews. Akasema, “Aisee, ngoja kidogo hapo, mhubiri.” Yapata majira kama haya ya asubuhi, nadhani. Basi akasema, “Ngoja kidogo hapo, mhubiri.” Akasema, “Kwani—kwani unaenda wapi?”

Nikasema, “Kwenye duka la vyakula.”

Kasema, “Hivi huna aibu?”

Nikasema, “Ati nini?”

¹⁹⁷ Kasema, “Kumwambia maskini yule mama pale anayekufa mle ndani, ya kwamba ataishi.”

Nikasema, “Vema, ataishi.”

Akasema, “Unajuaje kuwa ataishi?”

Nikasema, “Yesu amesema hivyo. Hiyo ndiyo sababu najua.”

Kasema, “Unajuaje?”

198 Nikasema, “Alinionesha ono lake.” Jinsi tu alivyofanya hilo; nilijua itakuwa hivyo. Hiyo ni kweli.

199 Akasema, “Ningejionea aibu.” Kasema, “Unazunguka tu na kuwadanganya watu namna hiyo.” Kasema, “Unapaswa kuona aibu. Sasa, najua kidogo ni vigumu kwangu, kwanza, kukutana nawe na kuzungumza nawe namna hiyo.”

200 Nikasema, “Hiyo ni sawa. Una mawazo yako mwenyewe, nami nina yangu, pia.” Nikapanda maskini baiskeli yangu nikaendelea.

201 Siku mbili baada ya hapo, mke wake, akiwa ni mwanamke Mkristo, akawa mgonjwa. Nikaenda kule, nikasema, “Bw. Andrews, naweza kukufanyia jambo fulani?”

202 Akasema, “Sasa angalia hapa.” Kasema, “Tunaye daktari mzuri.” Kasema, “Hatuhitaji msaada wowote kutoka kwako.”

203 Nami nikasema, “Asante.” Nikasema, “Najua una daktari mzuri.” Ndipo akalitaja jina lake; na yeye—yeye ni daktari mzuri hapa wa mjini, rafiki yangu. Nikasema, “Ni daktari mzuri.”

204 Akasema, “Ana kidole tumbo. Tutakiondoa, na hakuna lingine.” Kasema, “Hatuhitaji maombi hapa.”

205 Nikasema, “Haya, Bw. Andrews, sikuuliza hilo.” Nikasema, “Nilitaka tu kukwambia kuwa ni—ningeweza kukata kuni zako. Ningeweza kukufanyia chochote nilichoweza, kukuwashia moto, makaa, chochote ambacho ningeweza kufanya.”

206 Kwa hiyo, loo, alikuwa na madharau sana juu yake. Hakutaka, hakutaka uhusiano wowote na maombi. Nikasema, “Sawa.” Kwa hivyo nikarudi nyumbani.

Basi nilipofanya hivyo, mbona, wakampeleka hospitalini.

207 Basi kesho yake asubuhi, nikaanza kushika doria. Nilikuwa—nilikuwa mlinzi wa wanyama, mwajua. Nami nikajifungia maskini bunduki yangu, nikaanza kupanda barabarani. Nilikuwa nikienda zangu, kupanda barabarani, na kupitia huko.

208 Na muda si muda mwajua, pale, Kitu fulani kikaniambia, kasema, “Geuka urudi nyuma.” Huyo ni Yesu aliyefufuka, “Geuka urudi nyuma.”

Nikawaza, “Loo, vema, hilo, labda nilihisi . . .”

Kitu fulani kikasema, “Rudi nyuma.”

209 Nikageuka moja kwa moja na kurudi. Nikapigia simu Shirika la Utumishi wa Umma. Nilikuwa nikishika doria kwenye nyaya za juu, pia, kwa hiyo nikapiga simu, nikawaambia

sitafanya kazi siku hiyo. Kidogo kulikuwa na mvua ya manyunyu, ingawa si ya kutosha kunizuia kufanya kazi, lakini nikarudi tu nyuma. Sikujua kwa nini.

²¹⁰ Nikaketi na kuitenganisha maskini bunduki yangu, nilikuwa nimesimama pale nikiipiga msasa. Mimi. . . Meda akaniambia, mke wangu, akasema, “Kwa nini umerudi?”

²¹¹ Nikasema, “Sijui. Aliniambia tu nirudi. ‘Kutii ni bora kuliko dhabihu, kusikia kuliko mafuta ya beberu.’ Nimerudi tu.” Niliketi chini pale na nilikuwa nikipiga msasa maskini ile bunduki kuukuu.

²¹² Na muda si muda mwajua, nikaona, akipitia karibu na nyumba; na huyu hapa anakuja, na kofia yake imeinamishwa, mwajua, na kamasi ikining’inia kutoka puani mwake, naye akaingia. Akasema. . . [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Akasema, “Bibi Branham?”

Kasema, “Abe.”

“Je, mhubiri yuko hapa?”

Kasema, “Ndiyo.” Kasema, “Karibu ndani, Bw. Andrews.”

Kasema, “Aloo, mhubiri.”

Nami nikasema, “Habari za asubuhi, Bw. Andrews. Ketii.”

²¹³ Alisema, “*Mpfuuu!* U—ulisikia habari za Bibi Andrews?”

Nikasema, “La.”

Kasema, “Vema,” kasema, “atakufa, mhubiri.”

²¹⁴ Nikasema, “Loo, hiyo ni mbaya sana.” Nikasema, “Nachukia kusikia hayo.” Nikasema, “Ingawa, najua una daktari mzuri.”

Naye akasema, “Naam,” akasema, “lakini ha—ha—haikuwa ni kidole tumbo.”

Nami nikasema, “Ati haikuwa? Sicho?”

²¹⁵ Kasema, “La. Tuna mtaalamu pale sasa, kutoka Louisville.” Kasema, “Ni bongela damu. Liko saa chache tu kutoka moyoni mwake,” kasema, “linaelekea moyoni mwake.” Kasema, “Atakufa.”

²¹⁶ Nikasema, “Jamani, ni vibaya sana. Nachukia kusikia hilo.” Nikaendelea tu kupiga msasa bunduki yangu.

²¹⁷ Akasema, “Vema,” akasema, “vema, uh, yeye, uh, yeye ni mahututi sana.”

²¹⁸ Nami nikasema, “Naam, bwana.” Nikasema, “Hiyo ni. . .” Nikamwacha atoe jasho kidogo, kwa hivyo nikaendelea tu na kuendelea kuishughulikia bunduki yangu.

²¹⁹ Akasema, “Naam, uh, uh,” akasema, “unafikiri unaweza kumsaidia?”

²²⁰ Nikasema, “Mimi?” Nikasema, “Mimi si daktari. Sijui la kufanya, bwana.” Nikasema, “Mimi si daktari.”

221 Akasema, “Vema, uh, uh, unajua,” kasema, “uh, ni—ni—nilidhani labda—labda ungeweza, uh, kumsaidia kidogo.”

Nami nikasema, “Unamaanisha nini?”

222 Akasema, “Vema, uh, unajua, kama yule mwanamke kule chini kwenye. . .”

223 Nikasema, “Kumbe.” Nikasema, “Huyo hakuwa ni mimi. Huyo alikuwa ni Bwana Yesu.”

Naye akasema, “Vema. . .”

Nikasema, “Nilidhani hukumwamini?”

224 Alinisimulia hadithi ndogo wakati mmoja. Bibi ya—yake alikuwa na, ama shangazi ya—yake, naamini ndiye, alikuwa ametoa ahadi, angemlipa mhubiri mzee wa mzunguko dola tano mwishoni mwa mwaka. Alikuwa amefua nguo, wala hakuwa na pesa za kumlipa. Ndipo siku ya kufua ikafika, halafu mhubiri angekuwepo, naye hakuwa na pesa zozote. Naye alikuwa na shillingi, ama ndururu, ama chochote kilichogharimu kinoo kikubwa cha sabuni, naye akamtuma dukani. Akarudi, na kusema, alichukua kile ki—kinoo cha sabuni, na. . . na alikuwa analia. Kasema. . . Akanyosha mkono akachukua maskini aproni yake kubwa na kupangusa machozi.

225 Naye alikuwa kwenye lile birika la kale, kama ilivyowabidi mama zenu kufanya. Bila shaka, mnabonyeza tu kitufe sasa. Hayo yamepita, mnaona.

226 Lakini akaweka sabuni kwenye ubao wa kuoshea *hivi*. Na kuipaka; alisikia kitu kikisugua. Ikatokea kwamba aliangalia chini, na akatazama, hicho hapo kipande cha dola tano cha dhahabu, kimetokeza kwenye hicho kipande cha sabuni; alikuwa amemwahidi yule mzee mhubiri wa mzunguko. Akasema. . .

Nikasema, “Hicho kiliingiaje humo?”

Kasema, “Vema, ninashangaa tu?”

227 Nikasema, “Yesu aliyefufuka alifanya hivyo. Alitoa hiyo ahadi kwa moyo wote mwema. Alifikiri angeweza kufanya hivyo, naye Mungu alikuwa amemfanyia njia.” Jinsi tu anavyofanya mambo, ndivyo unavyomtambua. Kwa yale tu afanyayo, mambo anayofanya, jinsi anavyoyafanya. Akasema. . .

228 Akasema, “Vema, ni—nilishangaa, sikuzote.” Kasema, “Sikuzote imekuwa moyoni mwangu, nashangaa kama kulikuwako na. . .”

Nikasema, “Ati kama kulikuwako?” Nilisema, “Kunaye, Bw. Andrews.”

229 Akasema, “Vema, Ndugu Branham, unafikiri yeye. . . Ye—Ye—Yeye angeweza kumsaidia mke wangu?”

Nikasema, “Hakika. Najua anaweza.” Nikasema, “Hivi wewe. . .”

Akasema, “Je, utamwombea?”

²³⁰ Nikasema, “La. Wewe mwombe.” Nikasema, “Wewe ndiye utakayeomba.”

Akasema, “Vema, sijui jinsi ya kukariri sala.”

²³¹ Nikasema, “Huko hakutafaa chochote, kwa vyovyote vile, kama ukikariri sala.” Nikasema, “Piga magoti ukazungumze Naye.”

Akasema, “Vema, nifanyeje hilo?”

²³² Nikasema, “Sogeza tu kiti chako nyuma, na ukae tu pale. . . piga tu magoti pale juu yake, kando ya meza, uanze kuomba.”

²³³ Kwa hiyo akapiga magoti pale, akaanza kuomba. Naye akasema, “Sasa,” akasema, “Mista, sijui jinsi ya kuzungumza na Wewe.” Akasema, “Lakini laiti ungalimsaidia tu mke wangu!”

²³⁴ Akasimama na kusema, “Aisee, mhubiri, sasa hebu twende hospitalini tukazungumze Naye.” Kasema, “Labda, kama tukishuka hospitalini.”

Nikasema, “Sawa.” Mke wangu akajiandaa. Tukaenda huko nje.

²³⁵ Naye Bibi Andrews pale, hata usingeweza kuona macho yake tena, da—damu ilikuwa imetengana, wajua. Bonge la damu lilikuwa limesababisha damu. . . maji. Wala usingeweza kuyaona macho yake. Nikamwangalia. Loo, jamani! Mke wangu akaanza kulia.

²³⁶ Nikapiga magoti nikaanza kuomba. Nikasema, “Mungu Mpendwa, ninaomba sasa ya kwamba Wewe utamsaidia mwanamke huyu.” Nikasema, “Kwa kuwa sisi sote hatuna tumaini na hatujiwezi. Daktari amefanya yote anayoweza kufanya, na hata hivyo amelala hapa akifa.” Nikasema, “Ee Mungu, tungeweza kufanya nini? Tungewezaje kufanya lolote sasa? Tunakuita Wewe. Tunajua kwamba ulifufuka katika wafu, na U hai miongoni mwetu. Nawe unaonekana tu kama vile nuru inavyoonekana mikononi mwangu. Uko hapa. Nawe una uwezo wote, na unaweza kufanya hivyo. Sasa, Bwana, ikiwa tumepata kibali machoni Pako, tunakuja kwa unyenyekevu na kuomba rehema kwa ajili ya mwanamke huyu.”

²³⁷ Nilipokuwa nikiomba, mambo yakaanza kutendeka namna hiyo. Nikatazama na nikamwona akija nyumbani kwangu, akiwa na sambusa ya tofaa mkononi mwake, akanipa. Nami nikaketi kwenye baraza ya mbele na kuanza kuikata sambusa hii ya tofaa, na kuila. Nikasimama basi, akiisha kuonyesha lile ono.

²³⁸ Ilikuwa ni nini? Bwana aliyefufuka. Ilikuwaje? Yeye yuko miongoni mwa wanadamu. “Mambo niyafanyayo Mimi. . .” Alimwambia yule mwanamke dhambi zake, kisimani. Alielezea mahali Filipo alipokuwa, alipokuwa chini ya mtini, akiomba. Alijua mahali samaki alipokuwa, aliyekuwa na sarafu kinywani

mwake. Akasema, “Baba ananionyesha kazi, nami ninatenda kazi vile vile. Na mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya.” Ni nini? Ni ufufuo. Alifufuka katika wafu. Hajafa. Yuko papa hapa pamoja nasi sasa. Yeye ni halisi tu, chumbani, kama vile nuru ilivyo. Yeye ni halisi vile vile.

²³⁹ Mbona, mtu, miaka michache iliyopita, hakujua umeme ulikuwa ni nini, lakini alikuwa na njaa moyoni mwake kutaka kujua ulikuwa ni nini. Aliamini angeweza kuufanya umulike. Thomas Edison, naye alijaribu nyaya elfu kumi, lakini hata hivyo akapata kitu. Naye akaupa ulimwengu umeme.

²⁴⁰ Mwanadamu aliamini katika televisheni, na—na mambo haya mengine yote. Mungu aliyaweka yote hapa.

²⁴¹ Na kuna Nguvu za Kristo aliyefufuka asubuhi ya leo, papa hapa katika jengo hili, kumwoko kila mwenye dhambi, kujaza kwa Roho Mtakatifu, na kuponya kila ugonjwa uliopo ulimwenguni, ikiwa unajua tu waya sahihi ambao unaongoza kwake. Ni upendo na imani; huo ndio waya sahihi. Ingia ndani na usafiri mara moja, uone kama Yeye hasemi.

²⁴² Unajua, wakati Franklin alipoushika umeme, hakujua alichokuwa nacho. Alisema, “Nimeupata. Nimeupata. Nimeupata. Nimeupata.” Alijua kulikuwako na ufufuo. Kulikuwa na kitu alichokuwa amepata; hakujua ni kitu gani.

²⁴³ Labda wakati mwingine Roho Mtakatifu hunena nawe, hutajua tu ni nini; lakini unajua Yuko, jinsi tu Yeye anavyolifanya. Jinsi tu Mungu anavyofanya mambo; wanamtambua.

²⁴⁴ Huyu Bw. Andrews, basi, nilipotoka na kumwambia. Na siku ya tatu, yapata ninii mbili. . . Vema, yapata saa mbili tangu wakati huo, tukarudi nyumbani. Naye akaja. . .

²⁴⁵ Huu ulikuwa ni upungufu hapa, wakati huo. Alikuwa kwa miguu huko. Walikuwa wamemwita, wakasema, “Mke wako yuafa.” Kasema, “Ana ming’oroto ya mauti kooni mwake. Afadhali uje.”

²⁴⁶ Naye huyu hapa akarudi, amejaa masikitiko. Kasema, “Ndugu Branham,” kasema, “daktari alisema atakufa.” Kasema, “Yupo pale pale sasa. Akasema, ‘Atakufa.’”

Nikasema, “Lakini Bwana Yesu alisema, ‘Ataishi.’”

Kasema, “Vema, inawezekanaje. . . Kama akifa, anaweza kuishi?”

Nikasema, “Tayari yu hai.”

²⁴⁷ Haleluya! Usisisimkwe na *haleluya*. Inamaanisha “Mungu wetu asifiwe.” Kama kuliwahi kuwa na asubuhi ambayo haleluya zinapaswa kulia kutoka kwa watu, ni asubuhi ya leo.

Hiyo ni kweli. Mungu wetu asifiwe, kwa maana kila kivuli cha mauti kimeondolewa. Yu hai.

²⁴⁸ Angalieni. Naye akasema, “Vema, sasa,” kasema, “ataishije?”

²⁴⁹ Nikasema, “Mimi. . .Hilo si langu kupiga hesabu. Ni mimi tu kuamini kile ambacho Mungu alisema atafanya.”

²⁵⁰ Kwa hiyo basi alikuwa na huzuni kubwa. Ndipo baada ya kitambo kidogo akaenda hospitalini.

²⁵¹ Huyu hapa anarudi, akapitia kando ya nyumba, puu, puu, puu. Akaingia ndani mbio, akasema, “Mhubiri, unajua kilichotukia?”

²⁵² Nami nikasema, “Kitu gani, Bw. Andrews?” Nilikuwa bado nimeketi pale, nikiendelea kupiga msasa, mwajua.

Akasema, “Unajua kilichotukia.”

Nami nikasema, “Kwani imekuwaje, Bw. Andrews?”

²⁵³ Kasema, “Aliinuka. Maji yote yamemtoka. Akasema, ‘Nafa kwa njaa.’” Kasema, “Walienda wakamletea supu ya nyama. Akasema, ‘Sitaki supu ya nyama. Nataka nyama ya ndama na kabeji.’” Alikuwa na njaa.

²⁵⁴ Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni nini? Kwa sababu alifufuka katika wafu. Mwanamke huyo alitoka hospitalini akiwa mwanamke mzima.

Yu hai, Yu hai, kuleta wokovu!

Unaniuliza ninajuaje Yu hai? Anaishi ndani ya moyo wangu.

²⁵⁵ Hiyo ni kweli. Akaja karibu hapo. Basi siku tatu baada ya hapo, niliinyosha miguu yangu kwenye baraza ya mbele, nikala karibu sambusa nzuri sana ya tofaa, niliyowahi kula. Kwa nini? Yu hai. Alifufuka katika wafu.

²⁵⁶ Maskini mwanamke huyu hapa, alipoinuka kutoka kwenye kifua hicho kikuu, nayo hospitali ilisema atakufa. Alikuwa huku, kisha akakataa. Alifikiri ilikuwa ni ulokole, kuja kubatizwa.

²⁵⁷ Basi huku ameketi huko usiku mmoja, akiwa na homa kali, nyumbani kwake, angeweza kunisikia nikihubiri kule chini, kupitia nyumbani kwake. Nilikuwa nikihubiri juu ya ubatizo wa maji. Akasimama akaja, akayumbayumba akiingia kanisani. Naye alikuwa ameketi pale pale nyuma. Naye akasema, “Lazima nibatizwe.” Uvimbe mkubwa ulikuwa umevimba begani mwake. Bibi Weber, hapa, akaenda na kumchukulia vazi, akaja akamvika. Akaingia dimbwini, akiwa na homa, mia moja na nne, na akabatizwa mle kulingana na yale aliyomwahidi Mungu. Na leo hii. . .Hiyo imekuwa miaka kadhaa iliyopita. Na leo hii, huyo hapo, ameketi hapa, yu hai, asubuhi ya leo, ni kwa sababu Mungu yu hai na anamiliki, Naye alifufuka katika wafu.

²⁵⁸ Wiki chache zilizopita, yeye na binti yake walikuwa huko Louisville. Walikuwa wakishuka barabarani, na kulikuwako na maskini, mwanamke mzee ombaomba ameketi pale. Naye alikuwa akiomba. Kasema, “Mama, tafadhali nisaidie. Nina haja.” Akaangalia mfukoni mwake, alikuwa tu na pesa za kutosha, senti kumi na tano, naamini ndizo, wapate kuvuka daraja.

²⁵⁹ Alikuwa akienda zake. Akaanza kushuka barabarani. Bwana akamwambia, akasema, “Sasa, ulipokuwa hoi, nilikusaidia. Naye mwanamke yule yu hoi, nawe humsaidii.”

²⁶⁰ Alitembea mbele kidogo, akasema, “Bwana, lakini nina zile senti kumi na tano tu. Je, mimi na msichana wangu tutafikaje nyumbani? Tutafanyaje?”

Akasema, “Hiyo ni nini kwako? Nifuate Mimi.”

²⁶¹ Anageuka nyuma, anarudi nyuma. Akasema, “Mama, samahani.” Kasema, “Nina senti kumi na tano tu, ndizo tu nilizokuwa nazo, mimi na binti yangu tupate kuvuka daraja.” Kasema, “Nakupa wewe. Ndizo tu nilizo nazo. Nasikitika sina zingine.”

Akasema, “Bwana akubariki, binti yangu.”

²⁶² Akageuka, akaanza kutembea. Bintiye akasema, “Sasa, mama, tutafanya nini sasa?” Kasema, “Msongamano huo wote wa magari, itakuwa hatari kutembea kwenye daraja hilo.” Kasema, “Hatuwezi kutembea kwenye daraja hilo sasa.”

²⁶³ Akasema, “Sijui. Yeye aliniambia niende nikazitoe, na hizo ndizo tu nilizokuwa nazo.”

²⁶⁴ Wakishuka barabara, papo hapo ilitokea tu aliangalia. Binti yake akasema, “Loo, mama, tazama! Hii hapa ndururu.” Ikawa naye akaangalia, akasema, “Na hii hapa shilingi.”

²⁶⁵ Ni kitu gani? Jinsi tu anavyofanya mambo. Anatumjulisha kuwa yuko hapa.

²⁶⁶ Hapa kiangazi hiki kilichopita, nilikuwa nje, mikutanoni. Mke wangu akaingia, akasema, “Billy, sina budi kupata hundi. Sina budi kununua vyakula.”

²⁶⁷ Maskini mhubiri fulani mzee akapitia hapa, akasema, “Ndugu Branham, sina pesa.” Kasema, “Ni—nimefilisika. Sina budi kwenda Texas.” Kasema, “Ni—nitakulipa siku nitakapoweza.” Kasema, “Je, utanisaidia, nisaidie?” Kasema, “Nataka dola hamsini.”

²⁶⁸ Nikashuka kwenda kwenye benki, nione kama nilikuwa nazo. Naam, nilikuwa tu na—karibu tu mia moja, kwa hiyo nikaenda nikampa dola hamsini zake. Akazichukua akaondoka.

²⁶⁹ Mambo madogo yakiibuka, mnajua jinsi ilivyo. Mke akasema, “Billy, sina budi kupata hundi asubuhi ya leo, kama dola ishirini, sina budi kwenda kununua vyakula.”

Tukashuka kwenda kununua vyakula. Tukarudi. Akasahau mayai. Hatukuwa tukipata yoyote. Kwa hivyo nikawazia, “Loo, jamani, vema,” nikawazia, “labda mtu atafanya jambo.”

²⁷⁰ Kwa hiyo nikaenda kule, nami nilikuwa nikimsaidia Bw. May, kwa namna fulani nilikuwa... Hakukuweko na mtu nyumbani bado, nami nilikuwa nikiokota uchafu kwa sepetu kule. Ikawa niliangalia, ndipo nikaona gari kuukuu likiingia, likaingia kando, likasimama. Mhubiri mzee akatoka humo, kidogo ni kilema; ndipo akapanda juu, akaketi barazani, akaegemea nyuma. Nikawazia, “Maskini mhubiri huyo aliyevunjika; si—sina budi kwenda kumwona.”

Nikaenda pale. Nikasema, “Habari za asubuhi.”

²⁷¹ Akasema, “U hali gani, Kasisi Branham?” Kasema, “Sidhani kama unanifahamu.” Naye akaniambia yeye alikuwa ni nani. Kasema, “Mimi ni mmoja wa wahubiri hawa maskini.” Akasema, “Nilikuwa kule Cleveland, wakanipa petroli ya kutosha, kufika hapa.” Kisha akasema, “Gari langu kuukuu liko karibu kukauka huko nje.” Kasema, “Kitu fulani kiliniambia nipite hapa.” Kasema, “Labda ungenisaidia kidogo.”

²⁷² Nikamtazama. Nikawazia, “Jamani, uh,” mwajua. Niliwazia, “Maskini jamaa mzee.”

Nikasema, “Na tuombe.”

Akasema, “Nataka uombe. Nina nyonga mbaya.”

Nami nikasema, “Sawa.” Tukapiga magoti tukaanza kuomba.

²⁷³ Nilipoanza kuomba, Bwana akasema, “Mpe dola tano.”

²⁷⁴ Nikasema, “Vema, Bwana, bila shaka, Wewe unajua yote juu yake. Wewe, unajua kama ziko, ama haziko.”

Nami nikasema, “Bwana aliniambia nikupe dola tano.”

Kasema, “Hizo ni nyingi kupita kiasi, Ndugu Branham.”

²⁷⁵ Nikasema, “Lakini aliniambia nikupe dola tano.” Nami nikaandika hiyo hundi. Nikasema, “Ipeleke kwa Strother, watakupa pesa.” Nikawazia, “Sasa nini?” Akatoka nje. Akaondoka kwa gari, na alikuwa ameondoka kitambo kidogo.

²⁷⁶ Kulikuwa na mtu aliyekuwa akifanya kazi kwenye nyumba kule, akaja pamoja na Bw. Luther. Akasema, “Aisee, mhubiri!”

Nami nikasema, “Naam.”

²⁷⁷ Kasema, “Wajua,” kasema, “nina kuku mia moja nyumbani.” Kisha kasema, “Hao kuku wa siku nyingi,” kasema, “ni—ninawapa wote chakula cha kuanzia na chochote kile, na ulishaji, wala,” kasema, “siwezi kuvifanya vitu hivyo kutaga.” Akasema, “Karibu juma moja lililopita, nilishuka, nikasema, ‘Bwana, kama utaninii tu—ikiwa utawafanya kuku hawa kutaga, nitatoa nusu ya mayai na kumpa mtu.’” Kasema, “Unajua, wakaanza kutaga.” Kasema, “Kesho yake nikapata mayai tisini.”

Akasema, “Nina—nina kasha la mayai hapa, nataka kukupa.” Dola tano, hasa.

²⁷⁸ Ni nini? Jinsi tu Yeye anavyofanya mambo. Ninajaribu kusema nini asubuhi ya leo? Ninajaribu kusema hivi, ya kwamba, Yesu Kristo yu hai na anatawala. Amefufuka katika wafu. Aliumega mkate. Macho yao yakafumbuliwa. Wakatambua ya kwamba ilikuwa ni Yeye, jinsi tu Yeye alivyofanya jambo lolote. Angalia tunapoendelea nawe utagundua, jinsi tu anavyofanya mambo, Yeye angali hai na anatawala.

Yu hai, Yu hai, apate kuwapa wokovu!
Ati waniuliza ninajuaje Yu hai? Anaishi ndani
ya moyo wangu.

²⁷⁹ Ujumbe wake ulikuwa, “Nendeni mkawaambie wanafunzi Wangu nitakutana nao Galilaya.”

²⁸⁰ Na ujumbe Wake ni, leo, Yeye atakutana nawe. “Nitakutana nawe,” popote utakapokutana Naye. “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo.”

²⁸¹ Lakini, marafiki zangu, watu hao walishangaa, walipomsikia mtu huyu ufuoni, akisema, “Tweka wavu wako.” Hawakujua. Nao watu hawa wakienda zao Emau, walipotembea na kuzungumza Naye, wala hawakujua.

²⁸² Na wengi wetu, marafiki zangu, tumekosa ile mede ya wito mkuu katika Kristo, ni kwa sababu hatukutambua. Mara nyingi, kwenye Kizimba cha Hukumu, kutakuwa na masikitiko, unapotambua kwamba dini hiyo ya Yesu Kristo, inaleta wokovu na furaha na shangwe. Ambayo inaitwa, kama Paulo alivyosema zamani za kale, “Kwa njia inayoitwa uzushi.” *Uzushi ni* “wazimu,” mwajua. “Kwa njia iitwayo uzushi, ndivyo namwabudu Bwana Mungu wa baba zetu; kwa njia inayoitwa uzushi.”

²⁸³ Mara nyingi unaona watu wenye furaha na wanaoshangilia, na wamejaa Roho wa Mungu, ambapo uponyaji wa Kiungu na nguvu na maajabu na miujiza hufanyika. Wanasema, “Ni hiponozi.” Wanasema, “Ni *hivi, vile, au vinginevyo.*” Lakini, kama utasoma tu Biblia, ni Bwana Yesu Kristo. Kamwe humtambui. Kamwe hutambui Yeye ni Nani.

²⁸⁴ Ninatumaini ya kwamba kabla siku hii haijapita, kabla siku hii haijapita, ya kwamba atafanya jambo fulani maishani mwako, hata utamtambua, na ufufuo utachipuka moyoni mwako, kama bado haujachipuza. Na hebu... Nawe utaona ndege wakiimba tofauti. Yesu mpendwa aliyefufuka, asubuhi ya leo, amefufuka katika wafu, kwa hiyo hofu zote za mauti zimetoweka. Haleluya! Zimetiwa muhuri katika Bahari ya Usahaulifu.

²⁸⁵ Wakati maskini mtakatifu Paulo alipofikia mwisho wa safari, naye alikuwa ameketi pale na minyororo miguuni pake, na mikononi mwake; walikuwa wakitengeneza mikatale huko nje, ambapo watafikata kichwa chake. Waliposema, “Paulo, unafikiri nini kuhusu hilo sasa?”

²⁸⁶ Akasema, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; na tangu sasa nimewekewa taji ya haki, . . . Bwana, mwamuzi mwenye haki, atanipa Siku hiyo; si mimi tu, bali wale wote wanaopenda kuonekana Kwake.”

²⁸⁷ Walipomtoa nje kwenye gogo pale, naye akashusha ukosi wake, na kukilaza kichwa chake pale chini, mauti yalimkazia macho moja kwa moja usoni. Akasema, “Sasa nimekupata. Sasa unahofu.”

Akasema, “Ewe mauti, u wapi mwiba wako?”

²⁸⁸ Akaangalia huko nje, naye akawaona wakichimba lile shimo, wamtie kaburini. Lile kaburi la kale la matope likasema, “Nitakushika. Nitakufinyanga. Nitauchafua mwili wako. Mabuu ya ngozi yatatambaa ndani na nje ya mwili wako. Mimi . . .”

Akasema, “Kaburi, u wapi ushindi wako?”

²⁸⁹ Lakini akageuza kichwa chake kuelekea Yerusalemu, loo, jamani, “Lakini Mungu ashukuriwe atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo!” Loo, jamani!

²⁹⁰ Inanibidi kuja mwishoni mwa safari. Moja ya siku hizi, kazi zangu zitakwisha. Baadhi yenu nyinyi wavulana mlioketi hapa, ambao tulicheza pamoja, tukacheza ndondi pamoja, tukacheza gololi pamoja, na kila kitu. Tulikuwa wavulana wadogo wakati huo. Lakini sasa ninaanza kugundua . . . Kesho ni siku yangu ya kuzaliwa. Nitakuwa na umri wa miaka arobaini na nne, kesho. Mabega yangu yanaanza kuinama, na makunyanzi yanaingia chini ya macho yangu, nywele zangu zilizosalia zinaingia mvi. Ni nini? Mauti yanaingia; yanaendelea kunisaga.

²⁹¹ Lakini, ndugu, wakati mauti upande mmoja yanasaga, Uzima kwenye ng'ambo ya pili unafanywa upya tena. Hiyo ni kweli. Na moja ya siku hizi nyote mtasimama hapa makaburini, ambapo waliyapanga; na kama nikifa kabla Yesu hajaja, wataimba *Amini Tu*, “Mambo yote yanawezekana, amini tu.”

²⁹² Utakapowasikia wakisema, “ameondoka,” kisha wanyunyizie hayo madonge ya udongo juu ya jeneza; sijaondoka. Ni hai, bado, kwa sababu Yeye yu hai. Hapana.

²⁹³ Moja ya asubuhi hizi tukufu za msimu wa kuchipua, wakati yote yamekwisha; nayo mabomu ya atomiki tayari yameulipua ulimwengu na kuurusha huko ng'ambo, nao umezunguka-zunguka, kote katika miaka, na umetakaswa, ukarudishwa; nayo mitende itainuka tena duniani, ufufuo wa viumbe vyote, kama Mungu alivyofanya hapo mwanzo. Hakutakuwa na uchafuzi

wa udongo. Hakutakuwa na uchafuzi wa hewa. Nayo mitende, hakutakuwa na vijidudu wala magonjwa ya kuiharibu tena. Mitofaa haitazeeka kamwe. Haleluya! Itasimama. Na asubuhi fulani tukufu, nzuri, wakati ndege wakubwa wanaruka kutoka kwa mti hadi mwingine, Yesu ataonekana hapa duniani tena. Na atakapoonekana, “wale waliokufa katika Kristo, Mungu atawaleta pamoja Naye.”

²⁹⁴ Tutafufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, pia, tukutane na wapendwa wetu na kuwasalimu. Huo si utakuwa ni wakati mzuri sana? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁹⁵ Nami ninaweza kusimama kule... Na kumwona mama yangu mzee ameketi kule nyuma ya jengo, asubuhi ya leo, akizeeka na kutetemeka, na amejaa upoozi, naye anaanza kuzeeka. Ninapoweza kumwona pale, na kusema, “Mama, huyu ni mvulana wako.” Nami nafika pale na kuwaona wapendwa wangu, na marafiki zangu wapendwa walio hapa kanisani, maskini Ndugu George DeArk, wale wote walioshuka chini katika Kristo Yesu. Marafiki zangu wote wapendwa, watakapofufuka, nami ninaweza kukutana nao.

²⁹⁶ Na kisha niende huko na kusema, “Ni nani yule jamaa anayekuja pale?”

²⁹⁷ “Huyo ni Paulo. Huyu hapa Sila anakuja. Huyu hapa Danieli. Huyu, huyu hapa Ezekieli. Hawa hapa hao wengine wote.” Nasi tunaweza kushuka kupitia Paradiso hii ya Mungu.

²⁹⁸ Kutakuwa na ufufuo halisi, baadhi ya asubuhi hizi, rafiki. Tutakutana nawe.

²⁹⁹ Yule mtoto mchanga aliyekufa, mkubwa *hivi*, atakuwa msichana. Naye atamkumbatia mama yake, na kuomboleza huko na kulia, na kumsifu Mungu kwa ajili ya ufufuo Wake mtukufu wa Mwanawe, Kristo Yesu. Siku moja tukufu, itakuja.

³⁰⁰ Tumeishi sasa kwa sababu tuna arabuni ya wokovu wetu, Roho Mtakatifu hapa, akishuhudia ya kwamba kuna ufufuo. Ukoje?

³⁰¹ Wakati mmoja nilikuwa mwenye dhambi. Wakati mmoja singesimama nyuma ya mimbara hii. Wakati mmoja hungenisikia nikipaza sauti yangu na kusema “amina”; ningeona aibu kufanya hivyo. Kungekuwa na wakati mmoja nisingekuwa na tone la chozi machoni mwangu; ningeona aibu. Nilikuwa “Bill mkubwa mbaya.”

³⁰² Lakini, siku moja, Yesu Kristo alikutana nami katika Nguvu za kufufuka Kwake. Aliuponda moyo huo wa jiwe na kuutoa ndani yangu. Akaweka nia mpya. Akaweka asili mpya. Akaweka Mtu mpya humu ndani. Na leo hii, kwa sababu Yeye yu hai, mimi ni hai pia.

³⁰³ Na baadhi ya siku hizi, marafiki, nitakapofika mwisho wa safari, kama vile wewe tu na sisi wengine, na silaha zetu

zimechakaa sana, kutokana na vita! Loo, jamani! Angalia ile ngao ya kale, angalia ni mishale mingapi ya moto ambayo imenikinga nayo. Niko kule chini na ninahisi mawimbi yakiingia nafsini mwangu, najua niko mwishoni mwa safari basi. Kama tu mama yangu pale, na kama wote wa Branham, wanapozeeka sana, wanaanza kutetemeka kwa ugonjwa wa kutetemeka mwili.

³⁰⁴ Nataka kusimama pale, haleluya, nikiegemea ile fimbo, mwishoni mwa safari. Ninataka kutoa chapeo yangu, na kuiweka chini ufuoni mwa bahari; nipige magoti ufukoni, na kuuchomeka Upanga wa kale kwenye ala ya Umilele, na kuinua mikono yangu na kupaza sauti. Nami najua, ninapopitia kwenye bonde la uvuli wa mauti, ile Nyota ya Asubuhi itakuja kuiangaza njia. Roho Mtakatifu atatandaza mbawa Zake zinazometa-meta kuvuka Yordani ya kutisha iliyojaa matope, na kuzipeleka nafsi zetu zilizochoka kwenye nchi bora. Naam, bwana.

³⁰⁵ Usiogope. "Sitaogopa mabaya, kwa kuwa Wewe u pamoja nami." "Mauti yote yamemezwa katika ushindi." Kuna... Mauti hayawezi kufanya lolote. Mwandishi mmoja alisema, kwamba, "Kitu pekee ambacho Mungu alikuwa ameyafanyia mauti, aliyaweka kwenye gari la kukokotwa na kuyafunga nira, na kuyafungia kwenye magogo ya kufungia punda kwenye mkokoteni. Basi kitu pekee ambacho mauti yanaweza kufanya ni kumvuta mwaminio kumpeleka Mbele za Muumba wake." Hilo ndilo jambo pekee ambalo mauti yanaweza kufanya. Baadhi ya siku hizi, mauti yatasaga sehemu hii ipatikanayo na mauti.

³⁰⁶ Lakini nilipokuwa tu mtoto mchanga, na kulikuwa na kiumbe cha kimbinguni kikimngoja mama yangu, kunipa uhai, nilipozaliwa. "Basi maskani hii iliyo ya duniani ikiharibiwa, tayari kuna moja huko ng'ambo inayongoja Utukufuni," iliyowekwa tayari huko ng'ambo, ambako hakuna magonjwa wala mateso. Na kama tu vile nimezaliwa kwa Roho hapa, na Roho wa Mungu akilia, "Aba Baba"; si mimi tu, bali kila mtu ulimwenguni, ambaye amezaliwa mara ya pili, wakati huu—wakati mwili huu wa kiroho, huku tukikua katika neema ya Bwana wetu Yesu Kristo. Siku moja tutavuka mipaka kule na tutakuwa ndani ya mwili huo mpya, ambapo hakutakuwa na nywele zozote zenye mvi, mabega yaliyoinama, wala chochote kama hicho. Tutakuwa wachanga huko, milele, kwa sababu Yesu Kristo alifufuka siku ya tatu baada ya kufu-. . .baada ya kifo Chake, na akafufuka tena.

³⁰⁷ Yeye yu hai. Anamiliki. Sasa, nendeni mkawaambie wanafunzi Wake. "Nendeni mkawaambie watu Wake kwamba Yeye alisema, 'Nitakutana nanyi huko Galilaya.'" Moja ya siku hizi, katika Galilaya ya Mungu, huko ng'ambo mahali fulani, ninatarajia kukutana na Yeye katika amani, kwa sababu anaishi moyoni mwangu leo hii. Ninatumaini ya kwamba Yeye ni vile vile na kila mmoja wenu. Na wakati sisi. . .

³⁰⁸ Samahani nimechukua muda mwingi kupita kiasi hapa, yapata saa chache tu sasa hadi ibada ya shule ya Jumapili ianze. Na tuinamishe vichwa vyetu.

³⁰⁹ Ee Mungu wa Rehema, Muumba wa Mbingu na nchi, mwanzilishi wa Uzima wa milele, mpaji wa kila zawadi njema, tunakushukuru Wewe, asubuhi ya leo, kwa ajili ya kufufuka kwake Yesu Kristo. Miaka kama elfu moja mia tisa iliyopita, asubuhi ya leo, tukio hili kuu lilitukia. Watu walikuwa wanaogopa kifo kabla ya hapo; lakini, baada ya Yeye kuja, ndipo akaondoa hofu yote ya mauti.

³¹⁰ Na leo hii Yeye yu hai na anamiliki mioyoni mwetu. Alisema, baada ya kufufuka katika wafu, alisema, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu.” Miaka elfu moja na mia tisa na kitu imepita, tangu tukio hilo, lakini, asubuhi ya leo, Yeye yuaishi upya mioyoni mwetu.

³¹¹ Tumekusanyika hapa, asubuhi ya leo, Bwana, kumwabudu Yeye, kufundisha Neno Lake, kuhisi Roho Wake, kupeana mikono sisi kwa sisi; na kusema, “Bwana asifiwe,” sisi kwa sisi, kwa sababu tunaamini ya kwamba alikufa na akafufuka tena.

³¹² Tunaamini ya kwamba ndani yetu, asubuhi ya leo, Bwana, kwa neema ya Mungu, Uzima usiopatikana na mauti unamiliki miilini mwetu. Tunaamini ya kwamba mle ndani mna Roho wa Mungu asiyeweza kufa, ya kwamba hatakufa kamwe. Naye ameninii... Alisema, “Nitawapa Uzima wa milele. Hawataangamia kamwe, nami nitawafufua katika siku ya mwisho.” Tunaamini, Bwana, kwa sababu sisi ni mashahidi wa kufufuka Kwake.

³¹³ Sasa, Baba, tubariki siku nzima. Wabariki wageni langoni petu. Na jalia leo hii iwe siku ya furaha.

³¹⁴ Na kama kuna wale hapa, asubuhi ya leo, Bwana, ambao hawajapata kuzaliwa mara ya pili, ambao hawajui tukio la kuishi pamoja na Yesu katika Uzima uliofufuka, katika Maisha mapya, ambapo pingu za kale na tamaa zote za mambo ya ulimwengu zimetupwa chini, wala hawajui maana ya kuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu; Ee Roho Mtakatifu, uwashukie, leo hii. Pulizia ndani ya utu wao, Uzima usiopatikana na mauti. Na jalia kengele za furaha za Mbinguni zichipuke, katika Pasaka hii, habari njema za sikukuu, leo, na jalia watoke wawe viumbe vipya ndani Yako.

³¹⁵ Sikia maombi ya mtumishi Wako, Bwana, kwa maana ninaomba baraka hii katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Vema, na tusimame. Vema, Ndugu Neville. 

53-0405s Nendeni, Mkawaambie Wanafunzi Wangu
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org